# Mambo Yatakayokuwako

Rialto, California, USA

Desemba 05, 1965

1 Kwa Ndugu Boone na kusanyiko, hakika hili ni—ni majaliwa makuu kwangu kurudi San Bernardino tena. Mahali hapa panashikilia kumbukumbu nyingi kuu za siku zilizopita. Na mimi kusikia hayo, kutembelea hapa, na bado una ushawishi hai, mbona, hakika linakufanya ujisikie furaha kwamba Bwana alituelekeza kuja huku, miaka kadha iliyopita.

Nilikuwa tu nimeketi kule nje kwenye maegesho, sasa hivi, nikijaribu kukumbuka moja ya matukio yaliyotukia. Kulikuwa na Bibi Isaacson aliyekuwa mkalimani wangu huko Finland, kwenye kampeni ya Kifini, naye akaja kwenye gari nilipokuwa tu nikiondoka. Naye akasema, "Sauti yako ya Finland." Nami sijui tu kama Bibi Isaacson anaishi hapa. Sikujua. Asingeweza kuwepo usiku wa leo, nadhani? Bibi May Isaacson, naye anatoka Finland.

2 Halafu jambo lingine kubwa ambalo lilikuja kwenye kumbukumbu zangu, likuwa ni mhudumu mdogo katika mkahawa ambapo ninakula, mahali fulani karibu, wanapaita Antlers Hotel. Naamini hiyo ni kweli, sasa. Na maskini bibiye huyo alikuwa … Nilikuwa nikiomba pamoja naye. Alikuwa na ninii… Yeye, maskini bibiye mzuri, bali hakuwa Mkristo. Nilimwalika kwenye mkutano. Naye alikuwa amempoteza mtoto mchanga, nami naamini ya kwamba mumewe, walikuwa wametengana. Nasi tulikuwa tukiomba ya kwamba angepatana na mumewe, ama wangepatana, pamoja. Hivyo, sijui tu kama maskini bibiye huyo angeweza kuwapo. Unaona? Ninii …

Na kisha tukio lingine lililotukia, lilikuwa ni mtoto mchanga aliyeletwa kutoka mahali fulani, yapata mwendo wa siku moja. Naye alikuwa amekufa, na alikuwa amelala mikononi mwa mama. Naye alirejeshwa kwenye uhai. Je, hilo... Je, mtu huyo alikuwepo hapa? Na ikawa, naamini, kutoka kwenye jimbo hapa, ilikuwa ni juu hapa. Na maskini mama huyo alikuwa ameendesha gari usiku kucha, na baba, na maskini mama huyo akiwa ameketi pale, kwa huzuni, akimshika mtoto wake mchanga, mtoto aliyekufa. Nami nikawaza, "Imani kama hiyo!" Kama ningekuwa mnafiki mkubwa sana ulimwenguni, Mungu angaliiheshimu imani ya mama huyo.

Nikiwa nimemshika mtoto huyo mchanga mikononi mwangu, namna hiyo, nikiomba. Akapata joto, akaanza kusogea, akafungua macho yake madogo. Ninamrudishia mama yake. Kwa hiyo, walikuwa wametokea mahali fulani. Sidhani walikuwa Wapentekoste, hata hivyo. Walikuwa tu ninii … Ninaamini ilikuwa ni kanisa fulani tu, ambalo kutoka … Sijui hata kama walikuwa Wakristo, ama la. Sikuwauliza kamwe. Nilifurahi sana kuhusu mtoto huyo mchanga kufufuliwa tena.

Tangu wakati huo, Ndugu Boone, mambo mengi yametokea. Lakini tungali tunamtumikia Mungu yeye yule Ambaye anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele.

3 Nikiangalia tu kote, namwona Ndugu Leroy Kopp akiwa ameketi hapa. Ni mara ya kwanza kumwona kwa muda mrefu. [Ndugu fulani anasema, "Yeye ni Paul Kopp hapa." - Mh.] Paulo. Hiyo ni kweli. Leroy ni baba yako. Hiyo ni sawa. ["Na yeye—yeye yuko Urusi, usiku wa leo, kwa hiyo mwombeeni."] Loo, jamani! Urusi. Vema, hiyo ni, najua, askari huyu hodari pkue, yuko kule kwa ajili ya shughuli za Mfalme. ["Sawa."] Kwa hiyo, hakika nina furaha kuwa hapa na kumsikia huyu mhudumu kijana akisema alikuwa amevuviwa na huduma ambayo tulikuwa nayo tulipokuwa hapa. Hilo ni linafurahisha iliyoje!

Nami natumaini sasa, ya kwamba, nikijua tuna … Watu wamesimama, nasi hatutakaa muda mrefu sana. Tunazikumbuka zile ibada kuu za uponyaji.

4 Halafu, ninasikia ya kwamba kuna ndu—ndu—ndugu hapa jirani, mahali fulani, anayefanya kampeni ya uponyaji, Ndugu Leroy Jenkins. Naamini hilo ni kweli. Na hivyo nashukuru sana, nikitumaini ya kwamba Bwana anambariki na kumpa ibada kubwa, kubwa mno. Ni-…

Jamani, nilijisikia kuheshimiwa sana, usiku wa leo, kuja katika kanisa kama hili. Daima hujisikia vizuri zaidi kanisani kuliko ninavyojisikia katika hizo kumbi za kukutania. Hakuna kitu chochote dhidi ya ukumbi wa mkutano. Lakini, mnajua, mimi … Huenda ikawa ni ushirikina, ama ninaninii tu … Inaonekana kwangu kama kweli. Unaona? Wao … Unaenda kwenye hizo kumbi za mikutano ambako kuna mapigano ya ndondi, kushindana mieleka, tamthilia ya vichekesho, kila kitu kingine kinachoendelea, maroho machafu yanaonekana kubakia mahali hapo. Sasa, hilo linaweza kuonekana kama ushirikina, bali sivyo ilivyo. Lakini unapoingia kanisani, wewe … kwa kawaida, bila shaka kusanyiko la kiroho, inaonekana kama kwamba, hiyo ni kusema, u-unajisikia uko huru zaidi, kana kwamba kuna—kuna kitu fulani. Uwepo wa Mungu upo hapo. Unajua, panaonekana ni pa tofauti. Sijui jengo linaumba mazingira gani, lakini ni mahali ambapo watu wanakusanyika. Bila shaka, watu wale wale wako mahali pengine, bali kwenye hayo maeneo maovu. Huenda ikawa ni mimi tu ninafikiri hivyo. Lakini, hata hivyo, nina furaha kuwa hapa usiku wa leo.

5 Na sasa hatunaki kuwaweka kwa muda mrefu, kwa sababu ya wasikilizaji waliosimama. Nasi tunaenda, kesho usiku, mahali fulani pengine hapa. Hata sijui hiyo iko wapi. Iko karibu na hapa. [Ndugu fulani anasema, "Jumba la Mikutano la Orange." - Mh.] Wapi? ["Jumba la Mikutano la Orange Show."] Ukumbi Mikutano wa Orange Show, kwa ajili ya ibada kesho usiku. Mimi … Hii ni kati ya ninii,

ninazungumza kwenye ziara kwa ajili ya —ya kundi la Wafanyabiashara wa Injili Yote. Ambalo, nilikuwa na majaliwa ya kuzungumza kote ulimwenguni, kwa ajili yao. Na kwa hiyo humo, rafiki mpendwa sana alitualika hapa, nasi tuna furaha kuwa katika kusanyiko hilo usiku wa leo.

Sasa, kabla hatujafungua Biblia … Sasa, mtu ye yote aliye na nguvu za kimwili anaweza kuifungua namna hii. Unaona? Lakini inamhitaji Roho Mtakatifu kutufungulia Neno, kufungua ufahamu wetu na kuyafunua Maandiko. Naiamini Biblia. Naamini kwamba Hilo ni Neno la Mungu. Nami naamini ya kwamba dunia, ama watu wa duniani, watahukumiwa siku moja kwa Neno hili. Sasa, hilo linaweza kuonekana ni la ajabu. Sasa, kuna wengi wanaotofautina na wazo hilo.

6 Nilikuwa nikizungumza na rafiki yangu mwaminifu sana, si muda mrefu uliopita, ambaye ni Mkatoliki. Naye alisema, "Mungu atauhukumu ulimwengu kwa kutumia kanisa Katoliki." Kama hilo liko hivyo, ni kanisa Katoliki lipi? Unaona? Kwa hiyo, kama Yeye akiuhukumu kwa kutumia Methodisti, basi vipi kuhusu Baptisti? Unaona? Kama akiuhukumu kwa kutumia moja, hilo lingine limepotea. Hivyo, kuna mchafuko mwingi sana pale.

Lakini inatupasa tuliendee Hilo, tuone ninii yetu ka—lkauli yetu ya kweli, na Biblia inasema kwamba Mungu atauhukumu ulimwengu kwa njia ya Yesu Kristo. Naye ni Neno. Yohana Mtakatifu 1, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Na Waebrania 13:8 ilisema, "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Nami naamini jambo hilo kuwa ni Kweli. Sasa, ninaamini ya kwamba katika …

7 Mungu, hapo mwanzo, akiwa Mungu asiye na ukomo; Yeye ana ukomo na … ama hana ukomo, ndiyo namaanisha. Sisi ni wenye ukomo. Nia Yake ni kuu sana, nasi, katika nia zetu ndogo zenye ukomo, hatuwezi kuelewa hekima Yake kuu, isiyo na ukomo. Lakini basi, wakati Yeye anaponena jambo lo lote, linaweza kuonekana ni la ajabu sana kwetu, kumsikia akisema jambo fulani katika Maandiko, bali halina budi kutukia. Naamini ya kwamba Maneno Yake hayatapita kamwe. Kwa hiyo, ninaamini ya kwamba Mungu, akijua ya kwamba sisi katika akili zetu ndogo zenye ukomo tusingeweza kufasiri nia Yake—Yake kuu, Yeye hufasiri Neno Lake Mwenyewe. Yeye hahitaji mfasiri yeyote. Yeye hulifasiri Neno Lake Mwenyewe, kwa kulithibitisha Neno hilo katika majira Yake.

8 Naamini ya kwamba, Mungu, hapo mwanzo, ya kwamba Nuhu alikuwa Neno kwa ajili ya siku ile, kwa ajili ya Ujumbe Wake.

Sasa, baadaye akaja, baada ya huyo, akaja Musa. Sasa, Musa asingeweza kuchukua Neno la Nuhu. Asingeweza kujenga meli na kuwasafirisha majini kutoka Misri, kwenye Mto Nile, ama kwenda kwenye nchi ya ahadi, ama na kadhalika. Ujumbe wake haukufanya kazi katika siku ya Nuhu; hiyo ilikuwa ni sehemu ya Neno la Mungu lililothibitishwa kuwa Kweli na Musa.

Wala Yesu asingeweza kuwa na Neno la Musa. Na ninii … Luther asingeweza kudumisha neno la kanisa Katoliki. Wesley, asingeweza kudumisha Neno la Luther. Na Wapentekoste, wasingeweza kuchukua Neno la Methodisti. Wao … Unaona?

Kanisa linakua. Kila wakati, umetengwa katika Maandiko hapa. Hivyo, Mungu, kupitia Roho Mtakatifu, hulifunua Neno Lake, kwa kulidhihirisha na kulithibitisha, Mwenyewe, akionyesha ya kwamba ni Neno Lake likitimizwa katika siku iliyoahidiwa.

9 Yesu alisema hivyo. Yeye alisema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, amini kazi nizifanyazo," kwa kuwa zinashuhudia kwamba Yeye alikuwa ni Nani, mnaona, kama mtu yeyote angaliyajua Maandiko.

Sasa, Yeye alikuja kwa njia ya kipekee sana, ya ajabu sana, hata watu hawakutaka kumwamini, kwa sababu, "Yeye, akiwa Mwanadamu, alikuwa akijifanya Mwenyewe kuwa Mungu."

Kwa hiyo, Yeye alikuwa Mungu, kwa sura. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake."

"Na hakuna mtu awezaye kufanya kazi hizi pasipo Mungu kuwa pamoja naye," kama tunavyojua Nikodemo alisema hayo. Hilo, Baraza la Wazee liliamini jambo hilo.

Sasa, tunajua jambo hilo, hilo Neno. Laiti wangalilijua Neno! Yeye alisema, "Kama mngalimjua Musa, mngalinijua Mimi, kwa maana Musa aliandika habari Zangu." Nasi tunaangalia. Kama wangalikuwa wametazama huko nyuma katika Maandiko, kuona yale Masihi alipaswa kufanya, basi wangalimjua Yeye kwa uthibitisho, ya kwamba, "Mungu, kwa njia ya Kristo, alikuwa akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake," na kutimiza ahadi zote ambazo zilimhusu Masihi, ambazo Yeye alikuwa afanye. Yesu alilishuhudia Neno hilo, akilifanya Neno hilo liishi kwa ajili ya siku hiyo.

10 Nami ninaamini hilo ndilo jambo lile lile tunaloishi ndani yake leo hii: Mungu akishuhudia Neno Lake, kwa kuthibitisha yale aliyosema angefanya. Sasa, tunajua ya kwamba hii ni siku ya wokovu, ambapo Mungu anawaita watu kutoka ulimwenguni, kutoka kwenye maisha ya dhambi, kuingia katika maisha ya

utumishi. Na katika siku ambayo Mungu amemimina Roho Wake kutoka Juu, ishara kuu na maajabu yataambatana na huduma ya siku hii. Hii ndiyo… wakati mvua ya vuli na mvua ya masika zinanyesha, pamoja. Nasi tunajua ya kwamba kunapaswa kuwe na ishara kuu na maajabu. Ambapo, katika madhehebu mengi makubwa, Hili linakataliwa.

Lakini nashukuru sana kwa ajili ya milango hii iliyofunguliwa ambayo nimeipata, ya kuingia, na uvuvio unaotolewa kwa vijana wanaume kama vile mchungaji wenu hapa. Hilo limewafanya … Ninapoanza kuzeeka, na kujua ya kwamba siku zangu zinakwisha, na ninajua sasa kwamba hawa vijana wanaume wanaweza kuuchukua huu Ujumbe na kuueneza haraka hata kwenye Kuja kwa Bwana, kama Yeye hatakuja katika kizazi changu. Ambapo, ninatumaini kumwona Yeye. Ninamtazamia kila siku, nikikaa macho, nikijiweka tayari kwa ajili ya saa hiyo.

11 Sasa hebu na tuzungumze na Mwandishi kabla hatujasoma Kitabu Chake, tunapoinamisha vichwa vyetu.

Baba wa Mbinguni, tunakushukuru, sisi kuwa hai usiku wa leo, kurudi kwenye hili jiji kuu. Tukiwa tumeketi hapa katika mandhari hii ya milima, tukiangalia huko juu na kuona theluji, na maua ya rangi ya machungwa yakichanua, wakati uo huo, ni ulimwengu wa kupendeza iliyoje uliotupa wa kuishi! Na jinsi tunavyoona ya kwamba mwanadamu amevuruga na—na kutenda katika ulimwengu huu, linatufanya tujionee aibu, Baba.

Tuko hapa, usiku wa leo, kujaribu kutoa juhudi zetu, kujaribu kuwafanya watu waone jambo hili kuu ambalo Mungu amefanya, na kujua ya kwamba kuna kitu fulani kikuu zaidi tu ng'ambo ya pili. Jalia tutazame jambo hilo, usiku wa leo, Baba, tunapofungua Neno Lako na kusoma. Tunaweza kulisoma, Baba, bali hebu Roho Mtakatifu atufunulie Hilo kupitia ufunuo. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

12 Sasa, ninyi ambao labda mnataka kuandika mihtasari, na—na kusoma Maandiko pamoja na mhudumu, kama—kama kawaida wanavyolisoma Hilo kwa kawaida. Na ilikuwa kwamba kwa kawaida, wakati mimi … miaka kadha iliyopita, haikunilazimu kuandika Maandiko yangu, na kadhalika. Lakini nina umri mkubwa zaidi kidogo tangu wakati huo. Unaona? Ndiyo kwanza nipite miaka ishirini na tano, hivi majuzi tu, miaka ishirini na tano iliyopita. Hivyo, linakuwa kidogo si jambo zuri. Lakini bado ninajaribu kushikilia kila kitu ninachojua kufanya katika Neno Lake, mpaka atakaponiita.

13 Sasa, hebu na tufungue Yohana Mtakatifu sura ya 14, Maandiko tunayoyajua sana ambayo tunataka kusoma usiku wa leo, kutoa kutoka kwenye hili fungu la maneno, Bwana akipenda. Karibu nyote mnajua sura hili. Inaonekana kwamba, mara nyingi, inatumiwa katika ibada za maziko. Kulikuwa na wakati ambapo ningependa kuhubiri ibada ya maziko, ingelikuwa kwa huu ulimwengu. Hebu na ufe na uzaliwe mara ya pili. Yohana Mtakatifu 14:1 hadi 7, naamini, nimeweka alama hapa.

> *Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi.*
>
> *Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi: … kama sivyo, ningewaambia. Ninaenda na kuwaandalia mahali.*
>
> *… Nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena, niwakaribishe kwangu; ili kwamba nilipo mimi, nanyi mwepo.*
>
> *… Ninakoenda mnajua, na njia mnaijua.*
>
> *Tomaso akamwambia, Bwana, tunajua … uendako; na tunawezaje kujua njia?*
>
> *Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.*
>
> *Kama mngalinijua mimi, mngalimjua na Baba yangu; na tangu sasa mnamjua, na tena mmemwona.*

Bwana na aongeze baraka Zake kwa kusomwa kwa Neno Lake. Nasi tutalirejea tena, katika nyakati tunapoendelea, wakati tunapotaka kunena tu somo dogo kwa Kanisa.

14 Jana jioni, nilikuwa huko Yuma; Arizona, ambako ndiko nyumbani kwangu sasa. Mimi—mimi … Nilipokuwa hapa kabla sijaishi Jeffersonville, Indiana. Sasa nimekuwa huko Arizona, kwa ono likinipeleka kule, miaka michache iliyopita. Nasi tunaishi kule sasa. Sina kanisa lo lote kule.

Ndugu Green, ndugu yetu aliyeko hapa pamoja nasi, ameanzisha hekalu ambapo ninii … moja ya Assemblies of God, kanisa, assemblies ya mjini. Wameungana, nami nafikiri wote waliambatana na Ndugu Brock na Ndugu Gilmore, wakaliacha kanisa hili wazi. Na Ndugu Pearry Green, kutokea—kutokea Texas, aliingia na kupachukua mahali hapo, ambapo panashirikiana na sisi. Tunafurahi kujua ya kwamba—ya kwamba Ndugu Green amefungua tena kanisa hili lililokuwa limefungwa.

15 Na jana usiku, nilipokuwa nikizungumza huko Yuma kwa ajili ya Wanaume Wafanyabiashara Wakristo, nilizungumza juu ya somo la Unyakuo. Sasa, hilo huenda lilikuwa ni somo geni kuzungumzia miongoni mwa, kwenye dhi—dhifa, lakini karibu kila mmoja pale alikuwa ni Wakristo. Na hivyo ndivyo ilivyo kwenye hizi kampeni za namna hii, ama katika—katika kanisa. Ningeweza kusema sasa, "Ni wangapi wenu walio Wakristo?" Labda kila mkono ungeinuliwa juu. Wewe ni Mkristo. Na kwa hiyo, kama sisi ni Wakristo, nafikiri kwa namna fulani tunapaswa kuarifiwa hilo mapema. Haitubidi kukisia tu hilo. Tunataarifiwa mwisho wetu utakuwa ni nini.

Nami nataka kuzungumza juu ya jambo hilo usiku wa leo. Na somo litakuwa: Mambo Yatakayokuwako. Na sasa, nikizungumza jana usiku juu ya Unyakuo, kwa hiyo usiku huu, nataka kuzungumza juu ya somo hili, ili nipate kuliunganisha pamoja na Ujumbe wa jana usiku. Sasa, kutakuwako na Unyakuo, tunajua jambo hilo. Huo uko katika siku za usoni, zijazo.

16 Sasa, Yesu hapa anazungumzia, kuhusu, Yeye ametangulia kutuandalia mahali. "Msifadhaike mioyoni mwenu." Sasa, Yeye alikuwa akizungumza na Wayahudi. Kasema, "Sasa, ninyi mmekwisha kumwamini Mungu, niamininі na Mimi. Kama vile mlivyomwamini Mungu, niaminini na Mimi, kwa maana Mimi ni Mwana wa Mungu." Unaona? "Na, Mungu," kwa maneno mengine, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Baba Yangu anaishi ndani Yangu. Na yale mnayoona nikiyafanya, Mimi ninayafanya, si Mimi. Ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu. Yeye huzitenda hizo kazi."

"Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake."

17 Ilikuwa ni rahisi kwa hao Wayahudi waliokuwa wamefundishwa, katika vizazi na vizazi, kuamini kwamba kulikuwa na Mungu mkuu wa mbinguni. Lakini kuwazia kwamba Mungu huyo alikuwa ameshuka na alikuwa akijidhihirisha Mwenyewe kwa njia ya utu wa Mwanawe, Yesu Kristo, Mungu aliyefanyia hekalu ndani ya mwili wa nyama, hilo lilikuwa kidogo limezidi mno ufahamu wao ku—kuelewa.

Lakini Yeye alisema, "Sasa, kama vile mlivyomwamini Mungu, niaminini na Mimi. Kwa kuwa katika nyumba ya Baba Yangu mna makao mengi, nami naenda kuwaandalia mahali." Maisha ya Yesu yalikuwa yanakaribia kwisha, hapa duniani.

Alikuwa amewaonyesha watu, na kuwathibitishia, kwamba Yeye alikuwa ni Yehova aliyedhihirishwa katika mwili, kwa ishara kuu na maajabu, na katika kurejea kwenye Biblia ambayo aliyuwa ameirejea, kujirejea Mwenyewe. Naye alithibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, aliyedhihirishwa.

Sasa Yeye alisema, "Mnapoona maisha Yangu yakimalizika, yanamalizika kwa kusudi fulani. Nami ninaenda Zangu, kuwaandalia mahali; ili kwamba nilipo Mimi, nanyi mwepo." Kwa hiyo Yesu anawaambia wanafunzi Wake kwamba maisha haya hayaishii katika mauti.

18 Sasa, kwa kusema hili lilikuwa ni fungu la maneno la maziko. Kumbukeni, sisi, mauti yanaweka moja kwa moja mbele zetu, wala hatujui kama huenda kuna wengine katika jengo hili usiku huu ambao hawatatoka hapa wakiwa hai, katika maisha haya ya kimwili. Hivyo ndivyo jinsi yasivyo na uhakika. Dakika tano kutoka sasa, huenda ikawa kwamba vijana wadogo, wenye afya, vijana katika jengo hili wanaweza kuwa maiti katika dakika tano kutoka sasa. Hiyo ni kweli. Na tena, huenda ikawa, katika dakika tano kutoka sasa, kila mmoja tungekuwa Utukufuni. Hatujui tu. Hilo liko mikononi mwa Mungu. Yesu alisema Yeye hakujua, Yeye Mwenyewe, wakati huo ungekuwa lini, lakini, "Hayo yalikuwa mikononi mwa Baba peke yake."

Sasa, lakini, Yeye alikuwa akiwaambia, kwamba, baada ya kifo kuna kuishi. Kwa sababu, "Ninaenda na kuandaa mahali," hiyo ni kusema, kuwapokea, inaonyesha kwamba huko, Yeye alikuwa akizungumza nao, kwamba kulikuwa na—na maisha baada ya maisha haya kukoma. Na ni faraja ya jinsi gani hilo linapaswa kutupa sisi sote, kujua ya kwamba, baada ya maisha haya kwisha, kuna maisha, ambayo tunayaendea. Na unapozeeka, hilo linakuwa jambo halisi zaidi kwako. Unapoanza kuona siku za maisha yako zikikaribia, ndipo unaanza, unaanza kujiandaa vizuri zaidi, ukijitayarisha kwa ajili ya tukio hilo kuu. Sasa ni … Ni kuendelea kwa maisha haya haya katika ulimwengu mwingine, mahali pengine.

19 Kuzaliwa kwako hapa kulikuwa kumepangwa tayari. Nadhani unaamini jambo hilo. Kila mmoja wenu anajua ya kwamba kuzaliwa kwetu kulikupangwa kabla. Je! Ulijua kwamba kuwa kwako hapa kamwe hakukuanzia kwenye hadithi ya kutunga au wazo? Kila kitu kilipangwa na Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kwamba ungekuwa hapa. Mungu asiye na ukomo alijua. Na kule kuwa—kuwa asiye na ukomo, ilimpasa ajue kila kiroboto ambacho kingepata kuwa duniani, na ni mara ngapi kingepepesa jicho lake. Huko ni kutokuwa na ukomo. Unaona? Ninyi, akili zetu ndogo—zetu ndogo, haziwezi kuelewa kutokuwa na ukomo kunamaanisha nini. Mungu asiye na ukomo, Yeye alijua mambo yote. Kwa hiyo, hakuna kitu chochote kilichoenda kombo.

Kama tunajua Neno la Mungu, tunajua mahali tunapoishi. Tunajua saa tunayoishi. Tunajua kile kilichoko mbeleni. Tunaona yale tumepitia. Na Kitabu cha Mungu ni ufunuo wa Yesu Kristo; kazi Zake katika vipindi mbalimbali, hadi kwenye Kitabu cha Ufunuo, na kisha ahadi Zake zijazo. Kwa hiyo, ahadi

Zake zote ni kweli. Mungu hawezi kunena Neno lo lote bila Hilo kuthibitishwa. Kila Neno analosema halina budi kutimia. Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu …

20 Watu wengine wanachanganya Mwanzo, pale, wakati aliposema, “Mungu hujirudia Mwenyewe.” La. Ni kwamba tu, mnaelewa vibaya. Unaona?

Mungu, hapo mwanzo, Yeye alisema, “Na iwe. Na iwe. Na iwe.” Ulimwengu ulikuwa tu giza, katika machafuko. Hata wakati aliposema, “Iwe nuru,” huenda ilichukua mamia ya miaka kabla nuru kutokea. Lakini wakati alipolinena, halina budi kutimia. Haina budi kuwa hivyo. Unaona? Naye alinena Neno Lake. Mbegu hizo zilikuwa chini ya maji. Wakati alipoikausha nchi, ndipo hizo mbegu zikachipuka. Yale anayosema hayana budi kutimia.

Yeye alisema, kupitia kwa manabii. Nilirejea jambo hilo jana usiku. Kama vile, tumchukue Isaya, yeye alisema, “Bikira atachukua mimba.” Ni nani angewazia, juu ya mtu aliyeheshimiwa miongoni mwa watu, kusema neno kama hilo, “Bikira atachukua mimba”? Lakini kwa sababu yeye …

Nabii ni mwakisi wa Mungu. Yeye ameufanywa hivyo kwamba hawezi kunena maneno yake mwenyewe. Haina budi kuwa ni Maneno ya Mungu anayonena. Yeye ni kama tu anayeakisi, naye ni mnenaji wa Mungu.

Na kwa hiyo, basi, yeye alisema, “Bikira atachukua mimba.” Huenda asingeweza kuelewa jambo hilo, bali Mungu alikuwa amelinena hilo kupitia kwake. Kwa sababu, Yeye aliahidi kwamba, “Yeye asingefanya jambo lo lote mpaka awe amewafunulia watumishi Wake manabii.” Ndipo, wakati aliposema hilo, ilikuwa ni miaka mia nane kabla jambo hilo halijatimia. Lakini ilibidi itimie.

Hatimaye, hayo Maneno ya Mungu yalitia nanga katika tumbo la uzazi la bikira, naye akachukua mimba na kumzaa Imanueli. “Kwa ajili yetu M—Mtoto amezaliwa, tumepewa Mwana. Ataitwa Jina Lake, 'Mshauri,' 'Mungu mwenye nguvu,' 'Mfalme wa Amani,' 'Baba wa milele.'” Hilo ilibidi liwe hivyo, kwa sababu Mungu alikuwa amelinena kupitia kinywa cha manabii Wake. Na Maneno yote ya Mungu hayana budi kutimizwa.

Kwa hiyo, tunajua kwamba Yesu ameenda kuandaa mahali, ili apokee watu Kwake. Watu hao ni akina nani, natumaini ni sisi tulio sehemu ya hao watu usiku wa leo. Kama sivyo, rafiki yangu, Mungu amefanya njia, hali fulani, kwamba unaweza kujumuishwa katika hali hiyo kama ukitaka. Unao uhuru wa kujichagulia. Unaweza kutenda jinsi unavyotaka. Lakini sasa angalia, sasa, katika ulimwengu huu ujao. Kuna ulimwengu ujao.

21 Kama tu vile kuzaliwa kwako hapa, nilisema, wewe uliandaliwa. Mungu alijua wewe ungekuwa hapa.

Na sasa unajua, hata mambo ambayo wazazi wako walifanya, sasa, watu wanafikiri kwamba hayo hayapatilizwi kutoka kizazi hata kizazi, lakini yanapatilizwa.

Pale katika Kitabu cha Waebrania, naamini, kwenye sura ya 7, akinena, Paulo pale, hao waandishi, naamini ilikuwa ndio, alikuwa akinena juu ya—juu ya tukio kuu lililotukia pamoja kwa Abrahamu, kwamba alitoa zaka kwa Melkizedeki, wakati alipokuwa akirudi kutoka kumpiga yule mfalme. Na sasa yeye alisema, kwamba, “Lawi alikuwa katika viuno vya Abrahamu, wakati alipokutana na Melkizedeki, akitoka kuwaua hao wafalme.” Na ndipo akahesabu hilo kuwa “Lawi akitoa zaka, pia, wakati alipokuwa katika viuno vya Abrahamu,” babu wa babu yake.

Naye huzipatiliza dhambi za watu juu ya watoto wao—wao, kutoka kizazi hata kizazi, ambao hawatashikilia Neno Lake. Unaona?

22 Nyote mliandaliwa kabla na Mungu. Hakuna kitu kinachotokea kwa bahati, kwa Mungu. Yeye anajua yote kuhusu jambo hilo. Yote yamepangwa kabla, yamepangwa kwa vizazi vingi huko nyuma, ili kwamba uweze kuwa hapa usiku huu. Je! Ulijua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.” - Mh.]

Wazia tu, kwamba, wewe, wakati mmoja … Nitarudia jambo hili tena. Wewe, wakati mmoja, ulikuwa ndani ya baba yako, katika jeni ya baba yako. Sasa, yeye hakukujua wakati huo, wala hukumjua wakati huo. Lakini, unaona, ndipo uliwekwa kwenye tuta, katika tumbo la uzazi la mama, kupitia ndoa takatifu. Na halafu unakuwa mtu aliyedhihirishwa katika sura kama ya baba yako, ndipo kunakuwepo na ushirika.

23 Sasa, njia pekee unayoweza kuwa mwana, binti wa Mungu, kwa sababu huna budi kuwa … kuwa na Uzima wa Milele. Na kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, na huo ni Uzima wa Mungu. Aina moja tu ya Uzima wa Milele, huo ilikuwa ni Mungu. Hapo, kuwa mwana wa Mungu, ilibidi uwe ndani Yake daima. Jeni ya Uzima wako, Uzima wa kiroho, usiku huu, ulikuwa ndani ya Mungu, Baba, kabla hata ya molekuli haijakuwako. Unaona? Nawe si kitu ila ni udhihirisho wa chembechembe ya Uzima iliyokuwa ndani ya Mungu, kama mwana wa Mungu.

Sasa umedhihirishwa, baada ya Neno Lake kuja ndani yako, kukiangazia Nuru kipindi hiki. Unadhihirisha Uzima wa Mungu ndani yako, kwa sababu wewe ni mwana ama binti wa Mungu. Kwa hiyo,

mnapata kile ninachomaanisha? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Unaona? Wewe uko ndani ya … Sasa umefanywa, umeketi katika kanisa hili, usiku huu, kwa sababu wajibu wako ni kumdhihirisha Mungu kwa taifa hili na hawa watu, na ujirani huu ambamo unashirikiana.

Popote ulipo, Mungu alijua kwamba ungekuwa hapa, kwa sababu huna budi kuwa moja ya jeni Zake, ama sifa Zake. Ilibidi uwe hivyo. Kama uliwahi, kama unao Uzima wa Milele, basi daima ulikuwa ni Uzima wa Milele. Na Mungu, kabla ya kuwepo msingi, ulimwengu, alijua kwamba ungekuwa hapa. Na wakati Neno, ama maji, "kuoshwa kwa maji ya Neno" yalipokushukia—wewe, lilidhihirishwa katika kiumbe. Sasa una ushirika pamoja na Baba yako, Mungu, kama tu jinsi ulivyo nao na baba yako wa duniani. Unaona? Ninyi ni raia wa Mfalme; si raia, bali ninyi ni watoto, wana na binti za Mungu aliye hai, endapo kama Uzima wa Milele unakaa ndani yenu.

24 Sasa, basi, kama ilikuwa hivyo, Yesu alikuwa ni utimilifu wa Mungu uliodhihirishwa. Yeye alikuwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Kwa hiyo, wakati alipokuja duniani na kudhihirishwa katika mwili, wewe ulikuwa hapa ndani Yake wakati huo, kwa sababu Yeye alikuwa ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno; hilo Neno lilikuwa kwa Mungu, na Neno lilikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili, akakaa kwetu." Neno lilifanyika mwili. Kwa hiyo, wewe ulitembea pamoja Naye, wakati ulipokuwa ndani Yake, wakati alipokuwa duniani. Uliteseka pamoja Naye, na ulikufa pamoja Naye. Ulizikwa pamoja Naye. Na sasa umefufuka pamoja Naye, na ukadhihirisha sifa za Mungu, ukiketi katika sehemu za Kimbinguni; tayari umefufuliwa, umefufuliwa kwenye Uzima mpya, na umeketi katika sehemu za Kimbinguni katika Kristo Yesu. Loo, hilo linamaanisha mengi sana, siku hizi, enyi Kanisa! Hilo linamaanisha mengi sana kwetu, kujiona tumewekwa mahali petu ndani ya Yesu Kristo!

25 Sasa, kama sisi ni hizo sifa za Mungu, hatuwezi kuishi kwa kanuni za imani. Hatuwezi kuishi kwa njia ya udhehebu. Hatuna budi kuishi kwa Neno, kwa sababu Bibi-arusi ni sehemu ya Bwana Arusi, kama vile mke ye yote alivyo sehemu ya mumewe. Kwa hiyo, hatuna budi kuwa huyo Bibi-arusi aliye Neno. Na huyo Bibi-arusi Neno ni nani? Udhihirisho wa wakati huu, Bibi-arusi, si kanuni ya imani wala dhehebu; bali hekima kuu ya Mungu iliyo hai, sifa ya Mungu iliyo hai, kuuonyesha ulimwengu sifa za Mungu, katika kuumbwa kwa Bibi-arusi ambaye atadhihirishwa katika saa hii tunayoishi sasa.

Martin Luther asingeweza kudhihirisha sifa tunazodhihirisha, kwa sababu kwamba hayo yalikuwa pale mwanzoni, ule ufufuo, kama vile punje ya ngano iliyoingia ardhini.

26 Sasa, tunanukuu hili tena. Labda mlikisoma kitabu hicho, yule Mjerumani aliyekuwa akinidhihaki, na kusema nilikuwa mlokole asiyetumia akili kushinda walokole wote wasiotumia akili. Yeye alikuwa—alikuwa anapinga kabisa kila kitu kinachoitwa Mungu, na hata alimdhihaki Mungu. Kasema, "Mungu ambaye angeweza kuifungua Bahari ya Shamu na," kasema, "kuwatoa watu Wake; na kuketi akiwa ameweka mikono Yake kwenye tumbo Lake, na kuwaacha (katika nyakati za giza) watu hao wote wafe na kuteseka, hao watoto wadogo waliwe na simba."

Mnaona, mpango mzima—mzima, Kanisa lote, limejengwa juu ya ufunuo wa Kiungu. Yesu alisema, katika Mathayo Mtakatifu, ile sura ya 16, "Mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia jambo hili." Ilikuwa ni kitu gani? Ufunuo wa kwamba Yeye alikuwa ni Nani. "Na juu ya Mwamba huu, nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayataushinda." Unaona?

Ufunuo wa Yesu Kristo katika saa hii; si kile alichokuwa katika wakati mwingine! Kile alichokuwa sasa, Biblia inakidhihirisha. Kinakua ndani ya Bibi-arusi, kufikia kimo kikamilifu. Kwa hiyo, kama punje ya ngano, ya Kristo, ilibidi ianguke ardhini, vivyo hivyo ilimpasa Bibi-arusi kuanguka ardhini, kupitia nyakati za giza. Punje yo yote inayoingia ardhini haina budi kufa, la sivyo haitaweza kujizaa yenyewe, kujizaa yenyewe. Na lile Kanisa kuu alilolianzisha kwenye Siku ya Pentekoste, kwa kumtuma Roho Mtakatifu, ilipasa lipate kuteseka na kufa kifo cha kishahidi na kuingia mavumbini, kuingie ardhini katika ule wakati wa giza, ili lipate kuzaa tena katika wakati wa Luther, na kuja kwenye kimo kamili cha Bibi-arusi wa Yesu Kristo kwa ajili ya siku hii ya mwisho. Unaona? Hakuna njia …

27 Kwa hiyo, Bibi-arusi, katika Unyakuo, atatokea. Na ha yoyote yalipangwa kabla na Mungu, yote yameungwa mkono. Tangu mwanzo, Yeye alimjua kila mtu, kila mahali, ni nani angeketi, yote kuhusu jambo hilo. Yote yamepangwa kabla. Mungu alijua hilo lingekuwa hapa. Na—na wakati … Yeye aliifanya hivyo, ili kwamba tutakapofika pale … Yeye ameenda kutuandalia mahali. Na tutakapofika kule, yote yatakuwa yameandaliwa kama tu hata usiku huu ulivyoandaliwa, kama vile wakati huu ulivyoandaliwa. Naam. Kujua Kwake kukuu hapo kabla kunamwambia mambo haya yote, kwa kutangulia kujua.

28 Yeye yuko kila mahali kwa sababu anajua yote; anajua yote kwa sababu Yeye yuko kila mahali. Kwa hiyo, kwa kutangulia Kwake kujua … Sasa, Yeye hawezi kuwa tu kama upepo juu ya nchi, kwa sababu Yeye ni Kiumbe. Yeye si tu hadithi ya kubuniwa. Yeye ni Kiumbe. Yeye anakaa. Yeye hata anaishi katika nyumba. Yeye anaishi mahali panapoitwa Mbinguni. Na kwa hiyo, kwa kuninii Kwake, akiwa yuko kila mahali; akiwa anajua yote, akijua mambo yote, basi Yeye yuko kila mahali kwa sababu Yeye anajua mambo yote.

Wewe, sasa, ulikua kutokea kuzaliwa kwako, ulipozaliwa na ukawekwa kkatika huu ulimwengu. Mungu alijua kwamba ungekuwa hapa katika hii dunia, nawe ulikua tokea kuzaliwa hadi kufikia utu uzima. Mambo ambayo yalionekana ni ya ajabu sana kwako, katika usichana wako, uvulana wako, kama watoto, sasa yanaonekana halisi sana. Usingeweza kuyaelewa ulipokuwa mtoto. Lakini sasa, unapokuwa mtu mzima, unaanza kuelewa na kuona kwamba kila kitu kilikuwa kimewekwa tu sawa. Na, wewe, kweli hilo linamaanisha jambo fulani kwako sasa.

29 Hivyo ndivyo ilivyo katika kuzaliwa kwako kiroho. Unafanya mambo usiyoyaelewa, ukiwa mtoto mchanga, unakuja madhabahuni. Unayatoa maisha yako kwa Kristo. Unafanya mambo yasiyo ya kawaida. Unashangaa kwa nini ulifanya jambo hilo. Lakini baada ya kitambo kidogo, unapokomaa, kama Wakristo waliokomaa, ndipo unalielewa hilo. Unaona? Kuna kitu fulani kinachokua. Unaona ni kwa nini ilikupasa kufanya hivyo. Kuzaliwa kwako kiroho! Kuzaliwa kwako kimwili ni mfano wa kuzaliwa kwako kiroho.

Jinsi—jinsi ulivyokukaa, katika maisha haya, ulipokuwa unakua, kila kitu kiliendana vizuri kabisa, kwa sababu ulifanywa kwa ajili ya jambo hilo. Je! Halikuwa ni jambo la ajabu, usiku ule ulipoyumbayumba katika misheni, ule mkutano wa hema, ama lile kanisa dogo mahali fulani pembeni, na kitu fulani mhubiri alichohubiri, somo fulani, nawe ukaanguka moja kwa moja madhabahuni? Unaona? Unaona? Mungu alijua jambo hilo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Unaona? Hilo—lilionekana ni jambo geni kwako, kwa nini ulifanya hivyo wakati huo. Lakini sasa mnaelewa; ulijua kilichotukia. Linakukaa vizuri sana katika maisha haya, na itakuwa pia hivyo katika maisha yajayo. Ulimwengu huu na maisha yake yanaonekana ku—kusonga mbele unapoendelea kukomaa. Kila kitu kinaonekana kikienda sawa kwako.

30 Siamini katika ninii … ya kwamba mtu alitokea tu akawa hapa kwa bahati. Sasa hebu wazia tu, wakati ulipokuja u—ulimwenguni, kila kitu kilipaswa kutayarishwa kabla kwa ajili yako, ama kuandaliwa kabla, hasa, kwa ajili yako. Ni vigumu kwangu kufahamu jinsi ambavyo tungeweza kuwazia ya kwamba Mungu ambaye angeweza kututayarishia mambo haya yote mazuri asinge … tusingeweza kumtumainia. Kwamba, kama Yeye alituleta katika mchafuko huu tulio ndani yake sasa, na kutuandalia mambo mazuri ya maisha hapa, ni zaidi sana jinsi gani tunaweza kumtumainia kutayarisha mambo yajayo, unaona, mambo ya Milele! Inaonekana, nasema, kiajabu sana.

31 Nami si—sidhani kwamba Mbingu ni mahali ambapo mama yangu alikuwa akinisimulia habari zake. Naamini kwamba Kanisa limekua zaidi ya hapo. Kuwaziai, ilikuwa kwamba, miaka mia moja iliyopita, ama mia mbili, nafikiri watu wa kale walikuwa wakifikiri kwamba kila mtu aliyekufa alikwenda Mbinguni na alikuwa na kinubi, na—na kuketi juu kule mawinguni na—na kupiga kinubi. Sasa, walijua kwamba kulikuwa na mahali palipoitwa Mbinguni. Lakini, wao, kama hivyo ndivyo ilivyo, wanamuziki wote wangetushinda, unaona. Lakini sisi … Lakini si—si mahali pa namna hiyo. Si kupiga vinubi, hata kidogo. Naamini, siamini Biblia inafundisha jambo hilo. Lakini hiyo ilikuwa ni dhana waliyokuwa nayo kabla ya utimilifuu wa Neno kutokea, ama kule kufunguliwa kwa ile Mihuri Saba, ambayo tuliahidiwa katika wakati huu, jambo ambalo sasa tunalewa.

Naamini kwamba Mbinguni ni mahali halisi, kama tu vile hapa ni mahali halisi, unaona, kwa kuwa Mungu alituanzisha katika malezi yetu ya kiroho mahali hapa. Nami naamini kwamba Mbingu ni mahali halisi kama tu ilivyo hii hapa, ambapo hatuketi kule Milele na kuketi tu juu ya wingu. Hatupigi tu kinubi chetu, kote—kote hapa, daima. Lakini tunaenda mahali halisi ambapo tutafanya mambo, ambapo tutaishi. Tutafanya kazi. Tutafurahia. Tutaishi. Tunaelekea kwenye Uzima, kwenye Uzima wa Milele halisi. Tunaenda Mbinguni, paradiso. Kama tu vile Adamu na Hawa walivyoshughulika, na kuishi, na kula, na kufurahia, katika bustani ya Edeni kabla dhambi haijaingia, tuko njiani tukirudi moja kwa moja kule tena, sawa, moja kwa moja kurudi. Adamu wa kwanza, kwa njia ya dhambi, alitutoa nje. Adamu wa Pili, kwa njia ya haki, anaturudisha ndani tena; anatuhesabia haki na kuturudisha ndani.

32 Ninyi watu mnaochukua kanda sasa, juu ya ujumbe wa "kuhesabiwa haki," nawatakeni muuchukue. Nanyi mchukue kanda, nataka muuchukue huo. Nilizungumza juu yake, hapa wakati fulani uliopita.

Angalia jinsi mzazi wako wa duniani, kabla hujaja hapa, kabla hawajajua ya kwamba unakuja, walivyojiandaa kwa ajili ya kuja kwako. Wazia tu jambo hilo sasa, wazazi wako wa duniani. Ambapo, mzazi wa duniani ni mfano tu wa Mzazi wa kimbinguni. "Kama tunajua jinsi ya kuwapa watoto wetu vipawa vyema, ni zaidi sana jinsi gani Baba yenu wa Mbinguni anavyojua kuwapa watoto Wake vipawa vyema." Yesu alinena Maneno haya. Unaona?

Walijiandaa kwa ajili ya kuja kwako. Walitengeneza kitanda kidogo cha kulala, ama walichukuwa vidogo, viatu vidogo, na nguo ndogo, na kadhalika. Walitayarisha, kila kitu kwa ajili yako kuwasili, wakaviandaa kabla hata hujaja duniani.

33 Yesu ameenda kuandaa kuja kwetu kule. Sasa angalia. "Katika Nyumba ya Baba Yangu kuna makao mengi." Ama, hebu tuninii …

Simaanishi kuongeza kwenye Neno, wala kuondoa Kwake, kwa sababu hatupaswi kufanya hivyo. Ufunuo 22 ilisema, "Ye yote atakayeongeza neno, ama kuondoa Neno kutoka Kwake." Lakini hebu nifanye

hili tu, si kama kuongezea, bali ku—kuleta jambo fulani tu.

"Katika Nyumba ya Baba Yangu kuna aina nyingi za majumba ya fahari." Siamini kwamba tutakapofika Mbinguni kwamba kila mtu anafanana tu kabisa na mwingine. Siamini ya kwamba—kwamba wote watakuwa na nywele nzuri za njano, ama kahawia, ama—ama wote kubwa, au—au wote majitu.

Naamini kwamba Mungu ni Mungu wa vitu mbalimbali. Ulimwengu unathibitisha jambo hilo. Yeye ana milima mikubwa na milima midogo. Yeye ana nchi tambarare. Yeye ana majangwa. Yeye ana vitu mbalimbali, kwa sababu alikifanya jinsi alivyotaka. Naye alifanya majira; majira ya joto, majira ya baridi, majira ya kuchipua, majira ya majani kupukutika. Alifanya majira. Inaonyesha Yeye ni Mungu wa vitu mbalimbali. Yeye alikuumba wewe wa tofauti na mwingine. Baadhi ya watu wana kelele hasa; na wengine ni wa kushikilia kabisa; na wengine ni wazuri; wengine ni wema. Nawe unapata tu watu mbalimbali wa kila namna, na katika Ufalme Wake. Unaona?

34 Mwangalie Mtakatifu Petro, na umlinganishe na Andrea. Unaona? Andrea ndiye yule shujaa wa maombi, alidumu tu magotini mwake wakati wote. Na mtume Petro alikuwa mmoja wa vile vijinga vya moto viliyohubiri, na—na kadhalika. Na Paulo alikuwa zaidi sana kama msomi, zaidi sana kama … kama nabii, ama kitu fulani, na kujitenga.

Na, mnaona, Musa aliandika Vitabu vinne vya kwanza vya Kale. Ambapo, yeye aliandika Agano la Kale. Hivyo vingine vilikuwa ni torati, na wafalme, na zaburi, na kadhalika, na yale mtu fulani aliyoandika juu ya manabii. Lakini Musa aliandika zile torati, vile Vitabu vinne vya kwanza vya Biblia: Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, na Kumbukumbu la Torati.

Na halafu Paulo aliandika Agano Jipya. Hiyo ni kweli. Mathayo, Marko, Luka na Yohana waliandika matendo ya yale yaliyotukia, na kadhalika. Lakini Paulo alitenganisha torati na neema, na kuiweka mahali pake. Unaona? Yeye alikuwa ndiye mwandishi wa Agano Jipya. Yeye alitupa sisi maandiko ya Agano Jipya, akiweka Neno la Mungu katika utaratibu.

Sasa angalia, mengi, "majumba mengi ya kifahari," aina nyingi za majumba ya kifahari.

35 Kama vile, aina nyingi za vilima; kama, aina nyingi za mito, vijito, maziwa. Hayo yalikuwa hapa ulipokuja hapa, kwanza, kwa sababu wema wa Baba yako wa Mbinguni uliyaweka hapa. Kwa sababu, watu wengine wanapenda milima. Watu wengine wanapenda maji. Wengine wanapenda majangwa. Kwa hiyo, unaona, kuja kwako, Yeye alijua tabia yako na vile ungekuwa, kwa hiyo Yeye aliyafanya tu jinsi ambavyo ungeweza kuyafurahia. Loo! Nafikiri huyo ni Baba mzuri sana, unaona, tunajua kwamba Yeye aliyafanya namna hii.

Ninafurahi kwamba Yeye aliumba milima. Na—napenda milima. Mimi … Nami na—napenda hiyo. Ambapo, hao wengine, "Loo, siwezi kuvumilia … Loo, hapana shaka Yeye alimaliza kasha Lake la mota kule." Vema, Yeye aliimaliza ili nipate kuifurahia. Mnaona? Kwa hiyo basi wao wanasema, "Ninapenda nyanda, ambapo naweza kuona mbali sana." Vema, hizo tabia mbili tofauti, sote wawili tukiwa ni Wakristo.

Lakini Baba alijua ya kwamba ungekuwa hapa, na alikuandalia kila kitu kabla hujafika hapa. Amina. Kuja kwako mara ya kwanza, hapa, Yeye alitayarisha hilo kwa ajili yako wakati ulipofika hapa. Je, hilo si ni jambo zuri sana kuwazia yale aliyofanya?

36 Sasa, sasa, lakini kumbukeni, hizi ni karama za muda tu, katika mfano. "Sasa, tunajua kwamba Musa, katika kujenga lile hekalu jangwani, ama kuliandaa, alisema alifanya vitu vyote kulingana na ule utaratibu wa kile alichokiona Mbinguni." Unaona? Kwa hiyo, mambo ya duniani yanadhihirisha tu vile mambo ya Milele yalivyo. Na kama dunia hii tunamoishi leo, ikiwa ni kubwa sana, kama tunavyoipenda; na atunavyopenda kuishi, na kuvuta hewa, na kuona maua na kadhalika; kama—kama hiyo, kama hili hapa ndilo udhihirisho, ile inayokufa inadhihirisha tu ile iliyo ya Milele. Unapoona mti ukijitahidi, ukivuta, ukijaribu kuishi, hiyo inamaanisha kuna mti mahali fulani ambao haupaswi kufanya hivyo.

Unapomwona mtu hapa, akipambana apate kuishi, mtu fulani hospitalini, au katika kitanda cha wagonjwa, ama katika ajali, akipambana, na mkoromo wa kufa kooni mwao, na kuvuta, na kulia, na kuyalilia maisha kwa kupiga mayowe, hilo linamaanisha nini? Kuna mahali, mahali fulani, kuna mwili ambao haupambani na kulilia hayo. Unaona? Huo haufanyi hivyo.

Sasa, hizo ni karama zisizodumu kwetu, mambo haya, yanadhihirisha tu kwamba kuna Moja ambapo ndiyo ya Milele. Hayo ndiyo Yesu ameenda kuandaa, ile iliyo ya Milele kwa ajili yetu. Sasa, yanadhihirisha tu kuna yaliyo makubwa zaidi ya aina ile ile, maana haya ni ya aina ile ile.

37 Sasa, kumbukeni, Biblia ilisema, "Kama hekalu hili la makao yetu ya duniani, ikiangamia, ikiharibika, tunalo moja tayari linalongojea."

Kama tu vile mtoto mchanga, misuli yake midogo, ndani ya mama, inavyojinyonganyonga na

kujigeuka. Na, lakini … Unaona? Nawe unaona, unaweza kumchukua mwanamke, kama yeye anafoka sana; lakini anapokuwa mja mzito, punde kidogo kabla mtoto huyo hajazaliwa, kuna wema fulani unaomzunguka mwanamke huyo. Mkaribie, daima kuna kitu fulani, yeye ni mpole zaidi. Kwa nini? Kuna roho ndogo ya malaika inayongojea kuupokea mwili huo wa kawaida. Mara tu anapozaliwa, pumzi ya uhai humwingia. Na Mungu anaipulizia mle ndani, na anakuwa nafsi hai. Sasa, wakati tu mtoto huyu mchanga anapozaliwa, basi mwili wa kiroho upo pale kumpokea.

Na sasa, wakati mwili huu unapozaliwa hapa, katika dunia hii, kama vile mtoto mchanga anavyozaliwa, pia kuna mwili usiopatikana na mauti unaongojea kuipokea ile roho ndani yake tena. Loo, ni jambo kuu jinsi gani! Tuko—tuko sasa ndani ya Kristo Yesu, (amina), watoto wachanga, watoto wachanga katika Kristo, watoto wa Mungu, tukingojea ukombozi mkamilifu, kwenye Kuja kwa Bwana wetu Yesu, ninii … kutupokea juu Kwake Mwenyewe, wakati mwili , huu wenye kupatwa na mauti, utachukua kutokupatwa na mauti.

38 Mfano, mambo yote aliyofanya, yanadhihirisha mambo yajayo. Kama tu vile mwili unavyokupa hapa, kama tu mwili huu, aliokupa Yeye ili wewe uishi ndani yake, unaonyesha tu kwamba kuna mmoja aliye mkuu zaidi, bado, ujao. Unaona? "Kama tukichukua, ama tumechukua sura ya ule wa duniani, sisi pia tutachukua sura ya ule wa Mbinguni," ambao hauna maovu katika huu ujao. Sasa, huyu anashikilia uovu, magonjwa, mauti, huzuni. Nimeeleza tu hapa, si muda mrefu uliopita, nikihubiri juu ya Kubadilisha Umbo Kwa Neno La Mungu, jinsi ambavyo—kwamba mwili huu, una uovu ndani yake.

Na ustaarabu huu wote wa kisasa tunaoishi ndani yake ni wa ibilisi. Hamwamini jambo hilo? Biblia inasema ndivyo ilivyo; ulimwengu huu, kila serikali. Hatutaki kuamini jambo hilo. Lakini Biblia inasema jambo hilo waziwazi, ya kwamba kila serikali, kila ufalme wa dunia, unamilikiwa na Ibilisi na kutawaliwa na Ibilisi. Yesu alichukuliwa na Shetani, juu, na kumwonyesha falme zote za ulimwengu zilizokuwako, zitakazokuwako, na kadhalika. Naye Shetani alizidai, ni zake, wala Yesu hakubishana naye, kwa sababu yeye ni mungu wa ulimwengu huu. Unaona? Naye akasema, "Nitakupa Wewe hizo kama utanisujudia na kuniabudu." Unaona? Alikuwa akijaribu kumpa Yesu hizo, bila dhabihu. Unaona? Ilikuwa ni kupatana bei na Yeye.

Lakini ulimwengu ulikuwa umetenda dhambi. Kwa hiyo, adhabu ya dhambi ilikuwa ni mauti, na ilimpasa Yeye kufa. Hiyo ndiyo sababu Mungu alidhihirishwa katika mwili, apate kuchukua mauti juu Yake, apate kulipa adhabu. Hakuna kitu cha kurudi. Hakijatiwa alama. Imelipwa kabisa, bure. Deni lote limelipwa. Ni mali Yake sasa. Nasi ni wajumbe wa Ufalme Wake, tuliokusanyika hapa pamoja usiku huu, katika Jina la Yesu Kristo Mfalme wetu, tukiwa tumeketi katika sehemu za Kimbinguni.

39 Sasa, katika ulimwengu huu tunaoishi, hii elimu. Nataka kuwathibitishia. Elimu, sayansi, ustaarabu, na mambo haya yote ambayo yanaonekana sisi kuyafurahia sana leo hii, ni ya Shetani, nayo yataangamia. Unasema, "Ndugu Branham, ustaarabu?" Naam, bwana. Ustaarabu huu ulitokana na Shetani. Mwanzo 4 inathibitisha jambo hilo. Mwana wa Kaini, mnaona, alianzisha ustaarabu huu, akijenga miji, na vinanda, na kadhalika. Na ustaarabu ulikuja kwa njia ya maarifa. Maarifa ndiyo kile Ibilisi alichomuuzia Hawa, katika bustani ya Edeni, ambayo yaliyfanya kubanwa, kuvunja amri ya Mungu.

Kwa hiyo kutakuwa na ustaarabu katika ule ulimwengu ambao tunauendea, lakini hautakuwa ustaarabu wa aina hii, kwa kuwa katika ustaarabu huu tunayo magonjwa, huzuni, tamaa mbaya, mauti, kila kitu katika ustaarabu huu, kibaya. Lakini katika ustaarabu ule hakutakuwa na lolote la mambo haya. Hatutahitaji sayansi.

Sayansi ni upotovu wa kile cha asili, hata hivyo. Unaona? Unatenganisha molekuli, unatenganisha atomi na kufanya hivi-na vileI, kukulipua. Unachukua baruti, unagonga hiki, kuua kitu fulani. Unachukua gari. Na kutoa petroli kutoka ardhini, na mali ghafi kutoka ardhini, kulegeza uimara, ili dunia iweze kulipuka. Na unaendesha barabarani maili tisini kwa saa, na kumwua mtu fulani. Unaona? Loo, wasiwasi sana, kusongamana, kuharakisha; inatubidi kusukuma, kuchukua. Loo! Unaona? Yote ni ya Ibilisi.

Ufalme wa Mungu hautakuwa na magari, eropleni, wala mafanikio yoyote ya kisayansi. La. Haitakuwa na elimu yo yote, hata kidogo. Itakuwa ni elimu iliyo kuu sana kuliko hili, hata hii haitakumbukwa. Unaona? Elimu, ustaarabu, na haya yote, yanatoka kwa Shetani.

Sasa, unasema, "Ndugu Branham, kwa nini unasoma, basi?"

40 Unaona, ni kama tu, kwa nini ninavaa nguo sasa? Katika ustaarabu uliokuwa ukija, huo uliokuwa wa kwanza, hawakuhitaji nguo zozote. Walikuwa wametiwa utaji. Hawakuwa na sababu ya kuvaa nguo, maana hawakujua walikuwa uchi. Sasa ninyi … Sasa unaona, ya kwamba, sasa, basi, ya kwamba tunajua kwamba tuko—tuko—tuko—tuko uchi, dhambi inadumu hapa, basi inatupasa kuvaa nguo. Lakini haikuwa hivyo hapo mwanzo; hakukuwa na dhambi. Unaona?

Sasa, jambo lile lile liko katika namna ya ustaarabu, kwa ujumla. Tunasoma. Tunaandika. Tunafanya jambo hili. Lakini kamwe usizame kwenye jambo hilo. Kamwe usilifanye hilo kuwa mungu wako, kwa

maana huyo ni mungu wa ukomunisti. Unaona? Si la Yesu Kristo.

41 Yesu Kristo ni kwa imani; si kile unachoweza kuthibitisha kisayansi, bali kile unachoamini. Siwezi kuwathibitishia kisayansi, usiku huu, katika jengo hili, kwamba kuna Mungu, lakini hata hivyo ninajua Yeye yuko hapa. Lakini, kwa imani yangu, inathibitisha jambo hilo.

Ibrahimu asingeweza kuwathibitishia kisayansi kwamba atampata mtoto kwa mwanamke huyo, naye akiwa na umri wa karibu miaka mia moja. Lakini imani yake ililithibitisha. Unaona? Hakuhitaji uthibitisho wowote wa kisayansi. Mbona, ninii … Mbona, daktari angesema, "Mzee huyu ana kichaa, amekuja hapa akisema atapata mtoto m—mtoto kwa mwanamke yule; yeye akiwa na umri wa miaka mia moja, na huyo mwanamke tisini." Lakini, unaona, Mungu alisema hivyo, kwa hiyo halihitaji sayansi. Inahitaji imani, kuliamini Neno la Mungu, si sayansi.

42 Kwa hiyo, shule zetu na kadhalika ni hasara. Kama vile, Mungu kamwe hakusema, "Nendeni mkajenge mashule," ama hata, "muwe na shule za Biblia." Mnajua jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Yeye alisema, "Hubirini Neno." Hiyo ni kweli kabisa. Mifumo yetu ya elimu ilitupeleka mbali zaidi na Mungu kuliko cho chote nijuacho, hiyo ni kweli, mbali zaidi na Mungu. Si kujenga mashule, mahospitali, na kadhalika; hilo lilikuwa kwa ajili ya ulimwengu na kwa ajili ya kundi hilo. Lakini, sina kitu dhidi yao; wanafanya sehemu zao, lakini hilo bado silo.

Tunajenga hospitali, nzuri sana, na kutumia madawa bora sana tuliyo nayo, na maelfu hufa humo kila siku. Lakini, loo, jamani, katika Ufalme wa Mungu, hakuna mauti, hakuna huzuni. Amina. Hakuna haja ya mambo haya ya ulimwengu. Lakini tumepita kutoka kwenye jambo hili, kuingia katika kweli za Mungu; ambapo tunajitahidi sana kujaribu kupata mambo, kupitia sayansi. Na jinsi tunavyozidi kuwa wa kisayansi zaidi, tunajiletea vifo vingi zaidi. Tunapigana vita vya ambavyo tutashindwa kule, kwa hiyo achana nalo. Na kwa imani, mwaminini Yesu Kristo Mwana wa Mungu, usiku huu, na mumkubali. Yeye Ndiye.

Sayansi inakuandalia nini? Vifo zaidi. Hiyo ni kweli. Masputniki na kila kitu kikirushwa juu, na mambo haya yote, kusambaza mauti na kila kitu kote duniani. Usiangalie jambo hilo. Geuza kichwa chako juu zaidi ya hicho, kuelekea Mbinguni. Angalia mahali Yesu anapoketi, "Kwenye mkono wa kuume wa Mungu," usiku huu, "akiishi daima kutufanyia upatanisho juu ya maungamo yetu," yale tunayoamini, Neno Lake kuwa ni Kweli.

43 Sasa, tunaona, maisha haya yana kila namna ya maovu, kwa hiyo basi maisha yanayokuja hayatakuwa nayo. Haya yana tamaa mbaya, na maradhi, mauti. Kwa sababu, ni kitu gani? Siyo hiyo nyumba aliyokwenda kuiandaa. Hii ni nyumba ya magonjwa. Ni wangapi wanaojua nyumba ya magonjwa ni nini? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Hakika. Vema, hiyo ndiyo unayoishi ndani yake. Nyumba ya maradhi ni mahali wanapowaweka watu wote walio wagonjwa. Vema, hivyo ndivyo tu dhambi ilivyotufanyia, kutuweka katika nyumba ya magonjwa ya duniani. Kama ungekuwa … Wasingemruhusu mtu mwingine yeyote aingie kwenye nyumba ya magonjwa, kwa sababu kuna kila aina ya vijidudu vinavyoruka kila mahali mle, na—na watu watachukua vijidudu hivi na—na kuwa wagonjwa, wenyewe. Na dhambi ilituleta katika nyumba ya maradhi ya Ibilisi.

44 Loo, lakini hiyo nyingine inaitwa, "Nyumba ya Baba Yangu." "Nitaenda na kuwaandalia mahali. Kuwatoa kwenye nyumba hii ya magonjwa na kuwapeleka katika Nyumba ya Baba Yangu." Amina. Haya basi; niwatoe kwenye nyumba hii ya kale ya magonjwa ya kidunia. Yeye ameenda kuandaa mahali, mahali pakamilifu ambapo hakuna uovu uliopo, hakuna ugonjwa uliopo, hakuna uzee uliopo, hakuna mauti.

Ni mahali pakamilifu pakiwaita kwenye ukamilifu huo, nanyi hamna budi kuwa wakamilifu kufika kule. Biblia ilisema hivyo. Yesu alisema, "Iiweni basi wakamilifu, kama vile Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu." Ni Ufalme mkamilifu, kwa hiyo haina budi kuwa ni watu wakamilifu watakaokuja. Kwa sababu, huna budi kusimama na kuolewa na Mwana mkamilifu wa Mungu, nawe huna budi kuwa Bibi-arusi mkamilifu. Kwa hiyo unawezaje kufanya jambo hilo kupitia kitu kingine cho chote ila Neno kamilifu la Mungu, ambalo ni, "Maji ya utenganisho, yanayotuosha mbali na dhambi zetu"? Amina. Hiyo ni kweli. Damu ya Yesu Kristo, wazia jambo Hilo, inayotiririka, Neno likitoka Damu. Amina. Ile Damu, Ne—Neno la Mungu linalotokwa na Damu, ili kumwosha Bibi-arusi. Amina. Naam, bwana. Bibi-arusi anasimama mkamilifu, bikira, asiyeghoshiwa. Yeye hajawahi kutenda dhambi kamwe, kwanza. Amina. Alinaswa katika jambo hilo. Unaona?

Hiyo hapo Nyumba ya Baba ambayo ameenda kuiandaa.

45 Hii alikuja kwa kujuana kimwili, na kutokana na anguko, na haina budi kuanguka pamoja na kule kuanguka. Haijalishi utakitia viraka jinsi gani kitu hicho cha kale, kitaanguka, hata hivyo. Kimekwisha, kwa sababu kimehukumiwa, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Kimekwisha. Mungu atauangamiza. Yeye alisema hivyo. Kutakuwa na ukarabati wa kitu hicho chote. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]

Hapo mwanzo, wakati ulimwengu ulipozaliwa, wakati Mungu alipoyarudisha maji nyuma, kwanza,

kutoka duniani, kama alivyofanya kwa yale maji kutoka katika tumbo la uzazi la mama, kulikuwako na ulimwengu uliozaliwa. Naam. Na watu wakaanza kuishi juu yake wakati Mungu alipowaweka pale. Na ndipo wakaanza kutenda dhambi. Na ilibatizwa, kwa kuzamishwa, katika siku za Nuhu. Kisha ikatakaswa kwa Damu ya Muumba ikidondoka juu yake.

Na sasa hivyo ndivyo unavyokuja, kupitia kuhesabiwa haki, kumwamini Mungu. Ulibatizwa kwa toba, ama, pia, kwa ondoleo la dhambi zako. Ulikiri dhambi zako mbele za Mungu, Naye akakusamehe kwa ajili ya hizo. Nawe ulibatizwa, kuonyesha kwamba ulikuwa umekwisha, ulikuwa umesamehewa; ukikiri kwa watu, na kuuonyesha ulimwengu, kwamba unaamini ya kwamba Yesu Kristo alikufa kwa ajili yako. Nawe … Yeye alichukua mahali pako, na sasa wewe unasimama mahali Pake. Yeye alifanyika wewe, upate kufanyika Yeye.

Ndipo nguvu za Mungu zenye kutakasa ziliosha tabia zote zikatoka maishani mwako. Ulikuwa ukivuta sigara, ukinywa pombe, ukifanya mambo ambayo hayakuwa sahihi, ukisema uongo, kila kitu. Ndipo nguvu zenye kutakasa za Damu ya Yesu Kristo zinaingia maishani mwako na kukuondolea mambo yote mbali na wewe. Ikitokea ukasema jambo fulani si baya, haraka sema, "Ngoja kidogo. Samahani. Sikumaanisha kusema hilo namna hiyo." Unaona? Ibilisi ana mtego uliotegwa hapo. Lakini una neema ya kurudi, kama wewe ni Mkristo halisi, useme, "Nilikosea." Naam. Hivyo, kwa hiyo, sasa, ninii …

46 Sasa, jambo linalofuata unalopokea, lilikuwa ni ubatizo wa Roho Mtakatifu na Moto.

Sasa, Mungu, wakati huu Utawala wa Miaka Elfu utakapokwisha, Mungu ataupa ulimwengu ubatizo wa moto. Utakilipua kitu hicho chote. "Mbingu na nchi zitawaka kwa moto." Petro alisema hivyo. Na kitu hicho kitapata ubatizo wa moto, kufanywa upya kwa kitu hicho chote. Na ndipo kutakuwa na mbingu mpya na nchi mpya. Hiyo ni kusema, wakati, ambapo haki hukaa.

Hapo ndipo tulipo. Tumetoka kuwa viumbe vyenye kupatwa na mauti, kutoka viumbe vya wakati, kuwa viumbe vya Milele. Wakati Neno la Mungu lilipoziwasha nafsi zetu, nasi tunakuwa wana na binti za Mungu, tukiwa na zile sifa, jeni ya Mungu ndani yetu, kuwa wana na binti za Baba, Mungu aliye Mbinguni, tukilia, "Aba, Baba! Mungu wangu, Mungu wangu, katika Nyumba ya Baba yangu."

47 Sasa, ulimwengu huu wa kale hauna budi kuanguka, kwa sababu ulikuja kwa kujuana kimwili. Nao ilikuja kupitia katika kuasi, hapo mwanzo. Nasi tulizaliwa hapa kwa tendo la kujuana kimwili, kupitia kwenye kule kuanguka, na hauna budi kurudi moja kwa moja kwa njia hiyo, kwenye kule kuanguka. Lakini ule ambao Yeye sasa anakuandalia, hauwezi kuanguka, kwa sababu Yeye anaufanya uwe hivyo. "Nimeenda …"

Vipi kama ingalitupasa tu kudumu ndani ya mwili wa aina hii? Hivi huna furaha kuna kitu kama mauti? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Sasa hilo si ni la ajabu? Lakini sasa, tuseme, kwa mfano …

Miaka michache iliyopita, nilikuwa mvulana mdogo, na sasa mimi ni mtu wa makamo. Ninaye rafiki anayeketi moja kwa moja pale, Bw. Dauch, naye ana umri wa miaka tisini na mitatu, siku chache zilizopita. Mwangalie sasa. Miaka arobaini ama arobaini na mitano zaidi, huyo ingekuwa ni mimi. Sasa weka miaka mingine arobaini juu yake. Ungeenda wapi? Ninii pekee …

48 Nina furaha kwamba kuna kitu cha kututoa kwenye nyumba hii ya magonjwa. Kuna mlango uliofunguliwa, nao unaitwa mauti. Yesu anasimama katika mlango huo. Amina. Yeye ataniongoza kuvuka huo mto. Yeye atanipitisha kwenye mlango huo. Kuna mlango mkubwa unaosimama kule, unaoitwa mauti. Na kila wakati moyo wako unapopiga, wewe ni mmoja unayeukaribia huo. Na siku moja sina budi kuja kwenye mlango huo. Huna budi kuja pale. Lakini nitakapofika pale, sitaki kuwa mwoga. Sitaki kupiga makelele na kughairi. Nataka kufika kwenye huo mlango, nijifunike kwa mavazi ya haki Yake (si yangu), Yake.

Kwa hili ninajua, ya kwamba, "Ninamjua Yeye katika nguvu za kufufuka Kwake." Kwamba, wakati Yeye anapoita, nitatoka miongoni mwa wafu, kuwa pamoja Naye, kutoka kwenye nyumba hii ya magonjwa. Ko kote mwili huu unakoweza kuanguka, na ko kote unakoweza kuangukia, cho chote kile, nitatoka siku moja, kwa sababu Yeye aliniahidi. Nasi tunaamini jambo hilo. Naam, bwana. Yeye anaufanya Mmoja asioweza kuanguka.

49 Angalia jinsi mama mjamzito, duniani leo hii, jinsi mwili wa mama huyo unavyotamani vitu fulani. Nazungumza, nadhani na natumaini, kwa watu wazima wote watakaoelewa. Mama, katika kuzaliwa kwa mtoto mchanga, kama kuna kitu fulani kinachokosekena katika mwili wake, yeye huanza kutamani kitu fulani. Angalia jinsi baba …

Nakumbuka tulilelewa, fkama amilia maskini na—na karibu hatukuwa na kitu cho chote cha kula tulipokuwa watoto. Wengi wenu mliteseka kwa jambo hilo hilo.

Kwa hiyo jinsi ambavyo, wakati, kabla watoto hawajazaliwa, mama angetamani kitu fulani. Naye baba angetafuta kila mahali, kila kitu, ili kumpatia hicho. Unaona? Ni yeye, huo mwili, mwili wake, kalsiamu na

kadhalika ya mwili wake, na vitamini anazohitaji. Junie anatengenezwa, unaona, naye anatamani sana vitu, vyakula kwa ajili ya mtoto ajaye. Na jinsi ambavyo, wazazi, wanajaribu kulipata ili mtoto azaliwe kikamilifu na mwenye furaha iwezekanavyo. Unaona jinsi ambavyo wazazi wako watafanya jambo hilo? Wakati kuna kitu fulani kinachohitajika, mama anashuhudia jambo hilo, unaona, mfumo wake umeundiwa. Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Kwamba, jinsi ambavyo wakati kuna kitu fulani kinachohitajika hapa, kwa mtoto ajaye, yule—yule mama anaanza kukitamani sana hicho.

50 Sasa, ngoja kidogo. Kwa nini tuna miamsho? Kwa nini tunakusanyika pamoja? Kwa nini daima ninawakemea watu? Kwa nini ninawahimiza ninyi wanawake wa Kipentekoste: "Acheni kujipaka rangi, kujipodoa, na kukata nywele zenu, na vitu kama hivyo"? Kwa nini ninasema jambo hilo hivyo? Kwa sababu, njia ya mtindo wa kale ya pentekoste haikuwa ikifanya hivyo. Njia halisi ya Biblia si kufanya jambo hilo hivyo. Ninyi mnaovaa hizi kaptura na nguo ambazo zinawapasa wanaume, je, mnajua Biblia inasema ya kwamba hilo ni chukizo kwa Mungu? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Lakini tunaliruhusu hilo. Kwa nini Roho Mtakatifu anaendelea kukemea? Anajua kuna kasoro fulani pale. Lazima tuwe katika kimo kikamilifu cha Yesu Kristo. Hatuna budi kuwa wana na binti za Mungu. Lazima tutende kama watoto wa Mungu.

51 Muda mrefu uliopita, hadithi ndogo ilisimuliwa. Nilimwona ndugu mmoja mweusi ameketi huko nyuma. Huko Kusini, walikuwa wakiuza watumwa. Na jambo hili, wakati walipokuwa na watumwa kule, wakati utumwa ulipokuwa unafanyika, kabla ya ukombozi wa watumwa, wa lile tangazo. Nao wangepita kule na kuwanunua, hao watu, kama tu vile wangenunua ga—gari la mtumba, muuzaji. Walikuwa na risiti za mauzo, na wakawauza hao wanadamu kama tu walivyokuwa—walikuwa ni magari ya mitumba. Ulipata risiti za kuwanunulia.

52 Wakati mmoja mnunuzi alifika pale, dalali. Naye alikuwa anaenda kuninii … Yeye angezunguka kwenye mashamba haya makubwa na kununua watumwa. Naye akaja kwenye shamba fulani kubwa ambapo walikuwa na watumwa wengi, naye alitaka kuona walikuwa wanao wangapi. Na wote walikuwa huko nje, wakifanya kazi. Nao—wao walikuwa na huzuni. Walikuwa mbali na nyumbani. Walikuwa wanatokea Afrika.

Walikuwa wamewaleta hapa. Makaburu walikuwa wamewaleta huku na kuwauza kama watumwa, na kwa hiyo walikuwa na huzuni. Wanajua kamwe hawatarudi nyumbani tena. Wangeishi na kufa humu nchini. Nao walikuwa, mara nyingi, wangebeba mijeledi na kuwacharaza. Walikuwa ni mali ya huyo tajiri, naye alifanya nao yale aliyotaka. Nao walininii tu … Kama alikiua kitu hicho, alikiua. Na kama yeye, cho chote kile, alikifanya tu. Huo ni utumwa, kama vile Israeli ilivyokuwa, na—na mataifa mengi yalikuwa yameletwa utumwani. Nao ingewabidi kuwachukua maskini watumwa hao. Walitumikia tu. Walikuwa wakilia, mnajua, wakati wote, na wenye huzuni.

53 Lakini walimwona mmoja wa hao watumwa, kijana, alikuwa ameinua kifua chake mbele, ameinua kichwa chake juu namna hiyo. Haikulazimu kumcharaza. Haikulazimu kumwambia la kufanya. Hivyo huyo dalali akasema, "Nataka kumnunua yule mtumwa."

Akasema, "Hauzwi."

Akasema, "Ningetaka kumnunua."

Akasema, "La. Yeye hauzwi."

Kasema, "Je, yeye ndiye bosi wa hao wengine?"

Kasema, "La." Kasema, "Yeye si bosi. Yeye ni mtumwa."

Akasema, "Vema, labda unamlisha tofauti na unavyowalisha wengine."

Kasema, "La. Wote wanakula huko nje kwenye jiko la watumwa, pamoja."

Akasema, "Ni kitu gani kinachomfanya mvulana yule kuwa tofauti sana na hao wengine?"

Yeye alisema, "Hapa kuna jambo moja. Nilishangaa kwa kitambo kidogo, pia. Lakini mvulana yule, mgeni kutokea Afrika, bali huko Afrika baba yake ndiye mfalme wa kabila hilo. Na, ingawa, yeye ni mgeni aliye mbali na nyumbani. Yeye huenenda kama mwana wa mfalme. Yeye anajua kwamba, huko ng'ambo ya nchi, kwamba baba yake ndiye mfalme wa hilo kabila. Na sasa yeye anaenenda hivyo, kwa sababu anajua yeye ni mwana wa mfalme."

54 Loo, ndugu, dada, wewe na mimi, katika ulimwengu huu tunaoishi, hebu na tuenende kama wana na binti za Mungu. Sisi ni wageni hapa, bali tabia zetu zinapaswa kuwa kulingana na amri za Mungu, kwamba sisi ni wana na binti za Mungu. Tabia yetu, tunapaswa kutenda na kufanya, na kila kitu, kulingana na zile amri ambazo Mungu aliweka.

"Na ni chukizo kwa mwanamke kuvaa vazi linalompasa mwanamume." Ni kosa na ni dhambi, "Kwake kukata nywele zake," Biblia ilisema hivyo, "haimpasi hata kuomba."

Unasema, "Na *hili* je?"

55 Mtu fulani alinifuatilia; mhudumu mkubwa, mashuhuri, si muda mrefu uliopita. Kasema, "Ndugu Branham, njoo. Nataka kukuwekea mikono." Kasema, "Utaharibu huduma yako."

Nikasema, "Ati nini?"

Kasema, "Kuwakemea hao watu namna hiyo."

Nikasema, "Ninawaambia ninii …"

Kasema, "Naamini jambo hilo." Kasema, "Mimi ni Mpentekoste, pia. Naamini ya kwamba wanawake hawapaswi kukata nywele, hawapaswi kujipodoa, na vitu kama hivyo jinsi wanavyofanya, kupaka nyuso zao rangi." Kasema, "Hawapaswi kufanya hivyo. Lakini," kasema,"Mungu alikuita kuwaombea wagonjwa."

Nikasema, "Yeye aliniita nihubiri Injili."

Naye akasema, "Naamini jambo hilo. Lakini," kasema,"unafikiri *hivyo*?"

Nikasema, "Naam. Angalia mliyo nayo, mipango yote hii mikubwa, televisheni, na cho chote kile. Mimi sina kitu ila Mungu nitakayewajibika Kwake." Hiyo ni kweli. Nikasema, "Sina kitu ila Mungu nitakayejibu Kwake."

Yeye alisema, "Mi—mi—mi … Utaharibu huduma yako."

Nikasema, "Huduma yoyote ambayo Neno la Mungu litaiharibu, inapaswa kuharibiwa." Hiyo ni kweli. Hakika. Hiyo ni kweli kabisa.

Akasema, "Vema, utaiharibu."

56 Nikasema, "Ni nani atakayelisema Hilo basi? Unaona? Mtu fulani hana budi kulisema. Mtu fulani hana budi kutetea yale yaliyo Kweli, haidhuru inaumiza nini." Na marafiki, kama Mkristo, kama watu wanaoamini tunaenda Mbinguni, Roho Mtakatifu Mwenyewe atatufananisha na Neno la Mungu.

Akasema, "Unajua unalopaswa kufanya?" Kasema, "Watu wanakuamini wewe kuwa nabii." Kasema, "Unapaswa kuwa unawafundisha wanawake hawa jinsi ya kupata karama za unabii na mambo kama hayo, na mambo makuu, mambo ya juu zaidi badala ya jambo dogo."

Nikasema, "Nitawafundishaje aljebra wakati hata hawawezi kujifunza ABC zao? Wakati ambapo hata hawatafanya jambo la kawaida, unaona, jambo la kawaida, utawaambiaje mambo ya juu?" Wakati hata hutaanzia kwenye … Unataka kufikia mwishoni mwa ngazi kabla hujafikia hatua ya kwanza. Hiyo ndiyo sababu unaanguka. Unaona?

Anzia pale chini, na uendelee kupanda moja kwa moja juu jinsi Mungu anavyokuongoza juu. Unaona? Rekebisha maisha yako na daima ufuate kila sehemu ya Neno ambalo Mungu amekuwekea ulifanye.

57 Sasa wazia jinsi ambavyo Mungu … Tunapaswa kuwa na tabia na kutenda kama Wakristo. Mwenendo wetu unapaswa kuwa kama Wakristo. Kwa sababu, sisi ni wageni hapa. Hapa si nyumbani kwetu. La. Tulikuwa tumewekwa tu hapa, kwa muda mfupi. Hatuna budi kuondoka, kila mmoja wetu, usiku huu.

Sasa wazia. Kama Mungu, katika rehema Zake, anamfanya mama, kabla mtoto huyo mchanga hajazaliwa, anatamani sana vitamini fulani, na maneno ya mama yanasema, "Baba, na—na—nataka tikiti, au tikiti maji. Nataka kitu fulani, kingine." Hakipatikani … Mbona, atafanya kila awezalo, kupata hicho, kwa sababu anajua kwamba anataka mtoto wake azaliwe mkamilifu awezavyo kuwa. Unaona? Naye atafanya kila kitu ambacho anaweza kufanya, ili akipate.

Ni zaidi sana vipi Yeye anavyoweza, kukipata! Yeye ni Muumba. Sasa wazia jinsi Yeye alivyo na uwezo, kutuandalia mwili, kuishi kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, kama tunataka kuishi. Kuna kitu ndani yetu, kinachohitaji, kuishi. Na kuna kitu fulani ndani yetu kinachotaka kufanya yaliyo sahihi. Ndipo Mungu atamwita mtu fulani jukwaani, ama mimbarani, ambaye atahubiri Kweli tupu. Kwa nini? Unaona? Inakuonyesha. Ndipo, kama wewe ni mwana halisi wa Mungu, unaanza kupiga kelele, "Mungu, ondoa *hilo* kwangu. Nitahiri mbali na *hapa*. Niondolee mambo *haya*." Kwa nini? Linahitajika kwa ajili ya Makao yako ya mbinguni unayoyaendea, ambako Yeye ameenda kuandaa. Huna budi kuwa Bibi-arusi Neno halisi wa Kristo.

58 Nilikuwa nikihubiri siku chache zilizopita usiku juu ya dhabihu, katika siku za upatanisho. Nilikuwa nikihubiri juu ya mahali pekee ambapo Mungu, Kanisa pekee ambalo Mungu atakutana na mwanadamu humo, na ambalo liko, Yeye alisema, mahali ambapo Yeye aliweka Jina Lake. Yeye alisema, "Sitakutana nao mahali pengine po pote ila mahali hapo, lango ambalo niliweka Jina Langu ndani yake." Sasa, Yeye hakutani na wewe katika lango la Kimethodisti, lango la Kibatisti, ama lango la Kipentekoste, ama lo lote la hayo. Lakini Yeye aliweka Jina Lake katika Mwanawe. Yeye alisema, "Nilikuja katika Jina la Baba

Yangu.”

Mtu yeyote huja, na mtoto yeyote, huja katika jina la baba yake. Yeye … Nilikuja katika jina la Branham, kwa sababu baba yangu alikuwa ni Branham. Nawe unakuja kwa jina lako kwa sababu hilo lilikuwa ni jina la baba yako.

Naye Yesu, yule Mwana, alikuja katika Jina la Baba. Naye alisema aliweka Jina Lake, “Katika lango hili nililoweka Jina Langu, hiyo ilikuwa ni ile dhabihu.” Na ndani ya Yesu Kristo ndipo mahali pekee ambapo utapata ushirika na kumwabudu Mungu.

Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa.” Hilo halileti tofauti yoyote. Huna budi kuwa ndani ya Kristo.

Mhudumu fulani wa kimadhehebu, hivi majuzi usiku, aliniambia, akasema, “Bw. Branham, angalia hapa. Yesu alisema, 'Yeyote aaminiye.' Biblia ilisema, 'Yeyote aaminiye kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, amezaliwa kwa Roho wa Mungu.'”

59 Nikasema, “Je! Biblia pia haisemi, ya kwamba, 'Hakuna mtu awezaye kumwita Yesu kuwa Kristo, ila kwa Roho Mtakatifu'?” Unaona? Huwezi kuifanya Biblia iseme uongo. Haina budi kushikamana moja kwa moja.

Kwa hiyo inakupasa kuzaliwa mara ya pili hasa, kwa Roho Mtakatifu kuwa ndani yako, ambaye anashuhudia, wewe mwenyewe, unajua ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu. Na basi kama wewe umezaliwa, na u sehemu; kama wewe ni mwana wa Mungu, katika Neno la Mungu; unawezaje kulikana Neno? Roho Mtakatifu anawezaje kukufanya uamini kanuni ya imani, kwamba inakupasa kufanya kitu kama *hiki*, wakati Biblia ilisema jambo fulani lingine? “Inatupasa kujiunga na kanisa, na kufanya *hili*, ama kufanya *lile*,” wakati Biblia inakwambia dhahiri la kufanya? Unaona? Na kisha unapoona Hilo, na unarukia moja kwa moja ndani Yake, uko sawa na Hilo wakati huo. Endeleeni tu kusonga mbele moja kwa moja, na linakua tu.

Kama vile ki—ki—kiini kinachoingia katika tumbo la uzazi la mwanamke mwenye yai. Na ndipo wakati yai hilo dogo linapoanza kukua, na linaanza kuleta seli zazi nyingine, halileti seli zazi moja ya binadamu, na seli moja ya mbwa, na seli moja ya ng'ombe. Linatoa seli zote za kibinadamu.

60 Na wakati mwana wa Mungu, wakati huyo aliyechaguliwa tangu zamani … Hilo ni neno baya la kutumia, bali ni Mungu. Hii hapa Biblia ya Mungu. Kujua kabla kwa Mungu kunaweza kuchagua tangu zamani, kufanya kila kitu kitende kazi kwa ukuu Wake. Wakati ile mbegu iliyochaguliwa tangu zamani, ambayo ulipaswa kuwa, na Mungu akakuita, na maskini hiyo mbegu ya kifaranga cha tai mle ndani iliposikia Neno la Mungu, itajenga juu Yake, Neno moja juu ya lingine, juu ya lingine , juu ya hilo lingine. Haitachanganyikana na kanuni yoyote ya imani.

Angalia. “Katika malango haya, kila siku, wanapaswa kula mkate mwembamba wa mviringo ulio mpya. Na hakutakuwa na chachu itakayoonekana miongoni mwao, katika siku hizo saba.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.” - Mh.] Zile nyakati saba za kanisa, basi, hakuna chachu, hakuna kanuni za imani, hakuna kitu chochote kitakachoongezwa. Haina budi kuwa ni mkate usiotiwa chachu kabisa. “Hakuna chachu yoyote itakayopatikana kati yenu, hata kidogo.” Chachu pekee, Neno Lenyewe, ni hilo pekee. Na Neno hilo ni Mungu. Naye Mungu alifanyika mwili, katika Utu wa Yesu Kristo, ambao, huo ndio Lango. “Hilo ndilo Lango nitakalokutana nanyi humo, kuabudu, mtakazipofuata amri za Mungu.”

61 Kwa hiyo, kama wewe umeninii, usiku huu, umekuja tu, useme, “Namtolea Yesu Kristo maisha yangu,” nawe kamwe hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu; ingia ndani Yake. Huna budi kufanya hivyo. Huna budi kukua ndani Yake. Mwombe Mungu alundike Neno juu ya Neno, namna hiyo, mpaka ufanyike kimo kikamilifu cha mwana wa Mungu, ama binti wa Mungu.

Kuchukua mambo ya ulimwengu? Yohana wa Kwanza unasema, “Ukiipenda dunia, ama mambo ya ulimwengu, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.” Umedanganywa. Una upendo wa ulimwengu pale, na umekudanganya, Ibilisi amekudanganya, kwa kulundika mambo pale, na kuonyesha. Unaona? Huwezi … Vema, basi, huwezi kuondoa Neno moja la Mungu kutoka kwenye Biblia.

Ni kitu gani kilichosababisha dhambi ya kwanza? Si kwa uongo mkubwa tu wa wazi, bali ni kwa sababu Hawa alielewa vibaya, ibilisi alimpotosha, Neno moja. Neno moja, lilivunja mnyororo, na akakataa kuchukua Neno moja. Huo ulikuwa ni mwanzo wa Biblia.

Yesu alikuja katikati ya Biblia. Yeye alisema, “Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.” Hilo ni Neno lote la Mungu. Je, mnaamini *Hilo* ndilo ufunuo Wake? [Kusanyiko linasema, “Amina.” - Mh.] Neno lote la Mungu.

Kisha, katika Ufunuo 22, Yesu alimjia Yohana, kwenye kisiwa cha Patmo. Naye Yesu, “Mimi Yesu nimemtuma malaika Wangu kushuhudia mambo haya.” Unaona? “Ye yote atakayeondoa Neno moja kutoka

kwenye Hiki, ama kuongeza neno moja Kwake, nitamwondolea sehemu yake katika Kitabu cha Uzima."

62 Si kusema tu, "Vema, na—namwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu." Hilo ni sawa. Basi hayo mengineoya Hilo kwenye hilo. Unasema, "Nimehesabiwa haki. Ninampa mhudumu mkono wangu. Namwamini Yesu Kristo." Basi huna budi kuzaliwa mara ya pili. Huna budi kujazwa na Roho Mtakatifu. Unaona? Endelea tu kuongeza, unapoendelea. Unakua katika kimo cha mwana na binti wa Mungu. Jamani!

Mungu, anaweza kutuandaa, na kutupa sisi shauku hiyo maishani mwetu, ya kwamba tunataka kuona kitu fulani. Ni wangapi humu ndani wanaomtaka Mungu zaidi? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Mbona, inaonyesha kuna Mungu zaidi kwa ajili yenu. Unaona? Malionea hilo shauku sana. Maumivu yenu madogo ya utungu wa kuzaa yanakuja. Unaona? Mnahitaji zaidi, ili kwamba tuweze kuwa na furaha, na kuwa huru, na wakamilifu. Hatuna budi kuwa.

63 Kama vile ile—ile—ile chembechembe ndogo ya uhai ilivyo … kifuani mwa Mungu, kama tu, na hiyo chembechembe ya uhai iko katika ninii … kifuani mwa mama. Mungu anakuza; na kwenda, ameenda, kutuandalia mahali, mahali pa Milele pamoja na Yeye Mwenyewe; si mahali ambapo kuna nyumba ya magonjwa, kufa, dhambi, uzinzi, na uchafu wa ulimwengu hapa. Kama nia yako iko kwenye hayo, inaonyesha kamwe haijawahi kukutana na Mungu. Unaona? Umechochewa. Una udanganyifu wa akili.

Unajiunga tu na kanisa na kusema, "Vema, mimi ni mfuasi wa *hili*. Mama yangu alikuwa mfuasi wa *hilo*." Huenda hilo likawa ni sawa katika siku za mama yako, bali tunaishi katika siku nyingine.

Ujumbe wa Wesley kamwe haunge- … Yeye asingeweza kumchukua Luther. Luther aliamini katika kuhesabiwa haki, lakini Wesley alikuwa na utakaso. Wapentekoste walikuja, hawangeweza kuchukua kuhesabiwa haki tu, utakaso. Wao, ulikuwa ni wakati wa kurejeshwa kwa karama. Sasa sisi tunaondoka kwenye hizo. Unaona?

Zile hatua tatu za ule—ule Mzabibu ukikua. Ya kwanza, ni jani dogo, Luther alikuja, kutoka kwenye yale matengenezo. Vema. Hayo yalikuwa ni shina. Angalia maumbile. Mungu na uumbaji hutenda kazi katika mwendelezo, kwa sababu Mungu yuko katika uumbaji. Unaona? Kilichofuata kuja, kile kishada, chavua, wakati wa Kimethodisti. Ndipo wakaja Wapentekoste, loo, jamani, kikamilifu kabisa, unaona, kama tu punje ya ngano inavyoonekana kama ngano kamilifu, punje ya ngano. Ifungue, hakuna ngano pale, hata kidogo. Ni kapi, mbebaji Wake, bali Uhai huo unatenda kazi mle wakati wote. Unaona?

64 Hao waliokuwa nyuma kule katika wakati wa Luther wanamkubali Luther. Uhai huo ulipita, lakini ulienda na kuunda madhehebu. Jambo la kwanza unajua, likawa tu kimadhehebu ambalo mwisho wake ni kuteketezwa kwa moto. Unaona? Shina linakauka; ni mbebaji tu. Baadhi yao wangali wanajaribu kukaa katika hilo shina la mbebaji la kale, hawajui kitu juu ya Mungu, wamekufa. Wanasema, "Vema, angalia, sisi ni jani. Tulikuwa katika Luther." Hiyo ni kweli. Lakini angalia mahali lilipo sasa. Unaona?

"Sisi tulikuwa Wamethodisti."

Na hata, "Tulikuwa Wapentekoste." Lakini angalia Pentekoste, jinsi inavyokuwa baridi na la kawaida, jinsi kila mtu anavyoondoka zake. Unaona? Ni kitu gani? Ilikuwa ni mbebaji wa Mbegu halisi. Unaona? Haya mengine yote yalikuwa ni wabebaji, bali yaliunda madhehebu. Kama ukisema, "Mimi ni Mpentekoste," hilo halimaanishi kitu cha zaidi kwa Mungu kuliko kama ungesema ulikuwa Mkatoliki wa Kirumi au Myahudi, ama cho chote unachoweza kuwa.

Huna budi kuzaliwa, Uhai ule unaokuja kupitia kwa yule mbebaji pale. Usikae katika shina. Usikae ndani ya mbegu. Nenda moja kwa moja kwenye sehemu kamilifu.

65 Sasa, kumbukeni, na kila matengenezo tuliyokuwa nayo, juu ya hao Walutheri wote na kadhalika, katika miaka mitatu waliunda madhehebu. Hiyo ni kweli. Kila uamsho ulileta dhehebu katika miaka mitatu.

Wazia huu umeendelea kirefu kiasi gani, miaka ishirini na kitu, na hakuna dhehebu. Kwa nini? Ni ile Mbegu, ikija, ikiumbika chini ya ganda, namna *hii*. Kuanikwa, sasa haina budi kukaa Uweponi mwa Mwana, ipate kuiva kuwa punje tukufu kama Ile iliyoingia katika ile ya kwanza. Kanisa halisi lililoingia ardhini, kwanza, linarudi moja kwa moja kupitia kwenye shina, litokeze, Kanisa lingine, wakati tingatinga linapokuja kulichukua Hilo. Uhai ulioshuka ukaingia ndani ya Luther, Uhai ulioingia katika Methodisti, Uhai ulioingia katika Upentekoste, utaingia kwenye punje. Wote utaingia moja kwa moja kwenye punje, na kutoka, ukiunda Mwili mkamilifu wa Yesu Kristo.

66 Kama tu vile jua linavyochomoza, asubuhi. Huwezi kuangalia maumbile yo yote isipokuwa yashuhudie juu ya Mungu. Huhitaji hata Biblia, kujua kuna Mungu. Jua dogo lililozaliwa, mtoto mdogo dhaifu. Yapata saa moja, linaenda, linanaanza kwenda shuleni. Saa nne au saa tano, limetoka. Adhuhuri, liko katika nguvu zake. Saa tatu alasiri, linaanza kuzeeka. Saa moja ama mbili, kumi na mbili … Saa kumi na moja au kumi na mbili alasiri, mgongo unaanza kuinama. Linakufa. Je, huo ndio mwisho wake? La. Linafufuka tena kesho yake asubuhi. Uhai, mauti, kuzikwa, ufufuo!

67 Angalia majani yakiota kwenye miti. Linachipuka, jani zuri, la kupendeza; linatoa kivuli; linazaa matunda yake. Halafu, jambo la kwanza unajua, msimu wa kupukutisha majani unaingia, unayafikia, mauti; unakimbilia moja kwa moja kwenye mzizi, kuingia ardhini tena. Je, huo ndio mwisho wake? Majira ya kuchipua yanayofuata unarudi moja kwa moja tena kushuhudia. Loo! Huo ni uhai unaodumu.

Lakini, ndugu, dada, tuna Uzima wa Milele. Tuna Uzima wa Milele kupitia kwa huyu Mkuu aliyekuja, akaondoka, anayeweza kutuandalia mwili. Na maumivu haya yanayoongezeka tunayoyasikia, kama vile ninyi wanawake mnavyojisikia kuhukumika kwa yale mnayofanya, ninyi wanaume mnaojishikilia kwenye mafundisho ya seminari, na kadhalika, nyote mnataka kusema, "Ni—ninakariri kanuni hii ya imani. Ninafanya *hili*." Lakini kuna kitu fulani pale pale ndani yako, unapoona macho ya vipofu yakifunguka; viziwi wakiele… kipofu. Mambo haya yote yaliyoahidiwa. Unaona Neno likihubiriwa katika nguvu Zake. Unamwona malaya, kutoka barabarani, akifanywa bibiye. Unamwona u—unamwona mlevi akitoka pale, na awe mtakatifu halisi wa Mungu. Jamani! Unaona? Kuna kitu fulani, Uzima mle ndani. Nawe unaanza kujisikia, "Vema, labda sipaswi kufanya hivyo." Lakini, unaona, ni kitu gani, ni kitu fulani ambacho Mwili wako kule ng'ambo unahitaji. "Fanya hima." Lakini Mungu ana vitamini papa *Hapa* ndani kwa kila sehemu ya Mwili huo. Yesu ameenda kuandaa mahali kifuani mwa Mungu; naam, bwana, seli zazi fulani ndogo, mwana wa Mungu, mwana mdogo ama binti mdogo wa Mungu.

68 Yesu aliomba tu jambo moja, katika maombi Yake kwa Baba. Unajua hilo lilikuwa ni nini? Jambo moja, baada ya dhabihu Yake yote aliyoitoa hapa duniani, maisha aliyoishi, njia aliyotembea. Aliomba jambo moja, "Kwamba nilipo Mimi, nao wawepo pia." Yeye aliomba ushirika wetu. Hicho ndicho kitu pekee alichomwomba Baba katika maombi, ushirika wenu milele. Ukitaka kusoma hili katika Yohana Mtakatifu 17, ile aya ya 24. Basi tunapaswa kuwa na shauku na Yeye kiasi gani? Kama Yeye ana shauku …

Sasa sikilizeni. Kama kweli umezaliwa kwa Roho wa Mungu, hilo linamaanisha kila kitu kwako. Unaona? Si kitabu fulani cha sheria. Huishi sheria zozote na kadhalika. Unaishi kwa neema ya Mungu, Roho wa Mungu.

69 Mara nyingi nimesema jambo hili. Kama mmishenari, ningekuwa nikienda nchi za ng'ambo. Vipi kama ningemleta mke wangu ndani, watoto wangu, "Sasa angalieni hapa, enyi watoto! Sikiliza hapa, Bibi Branham! Mimi ni mume wako. Usiwe na waume wengine wakati nitakapokuwa nimeondoka. Kama ukifanya hivyo, nitakuchuna ngozi nitakaporudi nyumbani"? A-ha. Unaona?

Nigonge mguu wangu chini kwa kishindo, "Enyi watoto, mnasikiai ninayosema?"

"Naam. Ndio, baba. Naam, baba."

"Hebu nisikie tu ukosefu wa adabu wowote? Unaona?" Unaona? Sasa, hiyo ingekuwa nyumba?

Sasa vipi kama yeye akisema, "Sasa, wewe umemaliza, bwana? Sasa nataka kukuambia jambo fulani. Bw. Branham, mimi ni mke wako halali wa ndoa! Usiwe na marafiki wengine wa kike unapokuwa umeondoka, ama"? Sasa, hiyo si ingelingekuwa nyumba kweli? Sasa, hiyo ingekuwa ni kitu fulani.

Hatufanyi hivyo. Nampenda, naye ananipenda. Wakati anapojua ninaenda, anajua siendi isipokuwa Bwana aniita niende. Tunakwenda sakafuni, na kuwakusanya watoto. Tunaomba. Nilisema, "Mungu mpenzi, mtunze maskini mwenzangu, watoto wangu." Wanasema, "Mungu, mtunze baba tunapoondoka, wakati yeye ameondoka." Na halafu tunapoenda huko …

70 Sasa, vipi kama nilifanya jambo fulani baya huko? Vipi kama nikifanya uovu, nifanye jambo baya? Nami nirudi na kumwendea maskini mke wangu, nisimame pale na kuuangalia uso wake unaopata unaopata makunyanzi, na nywele zake zikigeuka mvi, nikamwendea na kusema, "Mpenzi, nataka kukwambia jambo fulani. Unajua nakupenda."

"Hakika, Bill, najua unanipenda."

"Nakuambia kile nilichofanya. Nilimpeleka msichana fulani nyumbani." Ni—niseme, "Je! Utanisamehe jambo hilo?" Naamini angenisamehe. Kweli naamini. Lakini je, ningefanya jambo hilo? Ninapotazama, nimesimama pale, ninaziona hizo nywele zikianza kuwa mvi, na kujua kwamba amesimama kati yangu na umma, nami najua amekuwa mke halisi jinsi gani, ningeweza kufanya jambo hilo? Ni—ni bora nife kuliko kumumiza. Ni bora nife.

Na kama hilo, katika upendo wa fileo kwa mke wangu, ni zaidi sana jinsi gani upendo wangu wa agapao kwa Mungu! Loo, nisingefanya lolote la kumuudhi Yeyeu. Hapana kwa kweli. Na—nampenda. Nataka kufanya kila kitu ambacho Yeye—Yeye anataka nifanye. Nataka kuenenda na kila Neno ambalo Yeye alisema, haidhuru ulimwengu unasema nini. Wao, wao hawataamini Hilo, hata hivyo. Nataka kujua yale aliyoniambia nifanye. Na kama nikikosa kitu fulani, ninamtaka anipe. Na kumwishia Yeye, tukijiepusha na ulimwengu.

71 Huu mwili wa kale wa kidunia hapa umefikia kwenye ninii… Hebu niwaambie. Mwili huu wa kidunia

ambao unauwazia mengi sana, ambao unaulinganisha na Hollywood. Unautunza sana. Haitakuwepo kirefu zaidi. Ukumbuke. Mmesikia ule unabii, mnaona, ambao Bwana alinipa, "Unaenda chini." Naam, bwana. Angalia. Utafanya hivyo. Angalia tu. Sasa, kamwe haikuniambia jambo lolote baya, bado. Nitamchukua hilo kwa mtu yeyote anayetaka kusema. Sijui ni lini ama wapi, bali umekwisha. Hukumu inaning'inia juu yake. Hakuna ukombozi kwa ajili yake; umepita. Unaona?

72 Sasa angalia jambo hili. Tuishi kwa ajili Yake, tukijiepusha na ulimwengu. Sasa angalia. Unaangalia kwenye televisheni, baadhi yenu akina dada, nanyi mnashuka kwenda hapa na mnataka, enyi wasichana. Ninyi ni vijana. Najua jambo hilo. Lakini ninyi ni Wakristo. Unaona? Ninyi mko tofauti. Hamtaki kuwa kama ulimwengu. Mnaupenda ulimwengu. Si ninyi vijana tu; baadhi yenu ninyi wazee. Unaona? Vema, ni kitu gani kinachofanya hilo? Unaona? Mnaangalia televisheni, mnakwenda dukani, mnaona maskini nguo hizi za kale ambazo wanawake huvaa, ambazo ni mbovu.

Je! Mnajua kitakachotekia kwenye ile Siku ya Hukumu? Huenda ukawa mwadilifu tu kwa mumeo kadiri uwezavyo kuwa, lakini katika Siku ya Hukumu itakubidi kuwajibika kwa kufanya uzinzi. Yesu alisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Ni nani wa kulaumiwa? Wewe. Unaona? Ulijianika mwenyewe, hizo kaptura na suruali.

Mwanamke fulani aliniambia, si muda mrefu uliopita, kasema, "Mimi sivai kaptura, Ndugu Branham. Namshukuru Bwana kwa ajili ya jambo hilo. Navaa suruali."

Nikasema, "Hiyo ni mbaya zaidi." Hiyo ni mbaya zaidi. Hiyo ni kweli.

73 Hata huwezi kununua gauni, ni vigumu, kwa ajili ya mwanamke. Akasema, mwanamke mmoja akasema, "Vema, ulisema kweli. 'Huwezi. Huwezi kuinunua.'" Lakini bado wanauza vitambaa na wanazo cherehani. Unaona? Kwa hiyo hakuna udhuru, hata kidogo. Unaona? Unaona?

Inaonekana, dada. Mimi ni ndugu yako. Nami ni mtumishi wa Kristo, ambaye hana budi kuwajibika kwenye Kiti cha Hukumu kwa yale ninayosema hapa usiku huu. Unaona? Utasimama, ukiwa na hatia ya uzinzi, kwa sababu kwamba upendo wa Mungu umevuja kutoka moyoni mwako. Ungali unaenda kanisani. Huenda bado ukacheza katika Roho. Huenda bado ukanena kwa lugha. Na mambo hayo ni sawa, bali hilo silo bado Sie. La, bwana.

Kumbukeni, Biblia ilisema, "Katika siku za mwisho watakuja Makristo wa uongo," si Yesu wa uongo. Wasingeweza kuvumilia jambo hilo. Lakini, "Makristo wa uongo," wapakwa mafuta wa uongo. Wamepakwa mafuta kabisa na Roho, kwa Roho Mtakatifu, na bado ni wa uongo. Unaona? Kuna mawili …

74 Wewe ni watu watatu. Sehemu ya nje ni mwili. Una hisi tano, ambazo unawasiliana na nyumba yako ya duniani nazo. Ndani ni roho. Kuna hisi tano pale, upendo na dhamira, na kadhalika, unawasiliana. Lakini ndani yake kuna nafsi.

Kumbukeni, "Mvua huwanyeshea wenye haki na wasio haki." Mvua ile ile itakayoifanya punje ya ngano kukua hufanya gugu kukua pia. Unaona? Ni kitu gani? Ndani ya mbegu hiyo kuna asili, na asili hiyo huonyesha, hujionyesha yenyewe. Inaweza kuwa katika shamba lile lile, papo hapo pamoja na gugu. Gugu na ngano vipo pamoja, vinashangilia vivyo hivyo. Kichwa chake kimeinama chini. Inakufa kwa kukosa maji. Wakati mvua inapokuja, gugu linaweza kupaza sauti kwa nguvu tu kama ngano iwezavyo. "Bali kwa matunda yao mtawatambua." Unaona?

75 Enyi Wakristo, huenda nisiwaone tena. Unaona, imekuwa miaka mingi tangu nilipokuwa hapa. Huenda nisiwaone tena. Lilinganeni Neno la Mungu. Angalia kwenye kioo.

Kama vile mvulana mdogo wakati mmoja, aliyekuwa huko mashambani, hajawahi kuona kioo. Yeye alikuja nyumbani kwa—kwa shangazi yake. Akaanza kupanda vipandio. Aliona kioo, naye akamwona mvulana mdogo kwenye kile kioo. Aliendelea kutembea, akiangalia. Na—naye angepunga mkono, na mvulana huyo mdogo angepunga. Naye akaendelea kuangalia. Yeye hakuwahi kujiona kwenye kioo. Kwa hiyo wakati alipokikaribia vya kutosha, aligeuka, akasema, "Mbona, Mama, yule ni mimi!"

Unaonekanaje, katika kioo cha Mungu? Je, kinaakisi binti ama mwana wa Mungu? Je, kuna kitu fulani, ambacho, ukisikia Hicho, je! kinakufanya umchukie mtu anayekisema Hicho? Ama je, kuna kitu fulani kinachovuta, kusema, "Najua mtu yule yuko sahihi kwa sababu hilo liko katika Maandiko"? Basi, hizo ndizo vitamini zinazohitajika kwa ajili ya mwili huu uliokusudiwa kuwa kule, nyumba ambayo huo mwingine atahitaji utakapofika kule. Unaona? "Nyumba hii; ikiwa tumechukua wa duniani."

76 Sasa kumbukeni, tunawazia sana huu mwili. Tunauvallisha nguo nyingi sana. Tunafanya mambo mengi sana, ambayo, yasiyo ya lazima, kubadili baada ya kubadili baada ya kubadili, na mambo haya yote. Na—na, loo, ni kila mtu tu.

Hebu tu mtu fulani aanzishe jambo fulani. Unapaka vipandio nyako rangi nyekundu na utazame akina Jones wakivipaka vyao rangi nyekundu. Ukibadilisha kutoka Chevrolet kuwa Ford, nao hawawezi kuvumilia

jambo hilo. Ni wakati wa kujilinganisha. Unaachilia ninii … Acha mwanamke fulani aje kanisani, amevaa kofia ya namna fulani, angalia wanawake wote wakiipata hiyo; hasa mke wa mchungaji, unaona, angalia tu kinachotokea. Sasa, hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Ni wakati wa kujilinganisha. Ndugu, inapaswa kuwa ni wakati wa kujilinganisha. Na yote hayo—mambo hayo yote ni—ni kwa kusudi fulani.

Sijali kama koti langu linafanana na suruali yangu. Nami nina wakati mgumu. Mke wangu ama binti mkwe wangu, mtu fulani, hana budi kuniambia ni aina gani—ya tai ya kuvaa nayo. Si—sijali kama zinafanana, hata hivyo. Nataka ujuzi wangu ulingane na Neno la Mungu. Hilo ndilo jambo lenyewe, maana hapo ndipo ninapokusudia kuishi; si kule pembeni na akina Jones, bali kule ng'ambo Utukufuni alipo Yesu, aliyeenda kutuandalia mahali. Naam, tunataka jambo hilo. Naam, bwana. Jiepusheni na haya yote.

77 Hili hekalu la duniani hapa, mnajua ni nini? Mwili huu ni kama koti la kale unalovaa, koti unalilovaa wakati mmoja. Lakini sasa una moja ambalo bora sana, hulitumii hilo tena. Unafanya nini? Unalitundika ndani ya kabati ya nguo, kwa maana unalo moja bora zaidi. Una koti bora zaidi. Ni la kisasa zaidi kuliko lile ulilokuwa ukivaa, lililochakaa. Nini? Ni lile vazi. Umo ndani ya hilo hapo. Vazi hilo lilifanya nini? Lilichukuua umbo lako. Unaona? Bali hulihitaji tena hilo sasa. Umeitundika. Ni tambara.

Na hivyo ndivyo mwili huu wa kale ulivyo, wewe, umechukua sura ya ule wa mbinguni. Hata hivyo, si wewe. Wewe uko ndani ya mwili huo. Wewe, Roho wa Mungu, yumo ndani ya mwili huo. Huyo ndiye anayefanya huo wa nje utii, kwa sababu ule wa ndani unauvuta, unaona, kuuleta ulilingane Neno la Mungu; ndani yako, wewe mwenyewe, utu wako.

Mwili huu ni koti tu la kale. Na siku moja, utafanya nini nao, kwa maana wewe ulikuwa—ulikuwa ndani ya vazi hilo kwa kitambo kidogo? Huo ni kama vazi la duniani; mwili huu. Mwili—mwili wako halisi, utu wako halisi, uko ndani ya koti hili la kale mnaloita William Branham, ama Susie Jones, ama ye yote yule. Unaona? Siku moja itaning'inia kwenye ukumbi wa dunia wa kumbukumbu yako. Utauweka huko nje kaburini, na mtu fulani ataweka jiwe la kaburi, "Hapa amelala Kasisi *Fulani*, ama Yohana *Fulani*, ama *Fulani*." Utalala pale kama ukumbusho wako. Watu walikuona tu katika jambo *huu*. Na kile ulichokuwa, wewe halisi, kilikuwa ndani ya huo. Lakini lile koti la kale, lenyewe, tu "lilichukua mfano wa lile la Mbinguni."

Loo, enyi watu, mmeshik nafasi ya kubadilisha makoti? Mmeshika nafasi ya Mbinguni? Kumbuka, ninyi hamna budi kuwa na nafasi zilizowekwa. Hamwezi kuingia bila ya hizo.

Ninazungumza nanyi katika lugha ya kisasa sasa, mnayoijua. Kama ukienda kwenye hoteli, useme, "Vema, nilikuwa na ninii …"

78 "Je! Mliweka nafasi? Vema, nasikitika. Kila kitu kimejaa." Uko huko nje kwenye baridi, kwa sababu ulishindwa kuweka nafasi.

Na kama ukifikia mwisho wa safari ya maisha yako, bila ya kuweka nafasi, hakutakuwako na Mtu pale wa kukulaki. Itakupasa kuingia katika Umilele wenye giza ambako kutakuwa na mayowe, na kulia, na kuomboleza, na kusaga meno. Huna budi. Huwezi kuuingia ule Mji, wewe, kwa sababu hujaweka nafasi. Humna budi kuweka nafasi, upate kuuingia ule Mji, ambako Yesu ameenda kuwaandalia mahali. Kumbuka, huna budi kujiwekea nafasi, na uwe umevaa vazi la wokovu. Huwezi.

79 Katika Mathayo, nina Andiko hapa. Ninaangalia Maandiko, Mathayo, ishirini- 22:1 hadi 14. Sina muda wa kulisoma, kwa sababu tumechelewa sana. Nimezungumza kwa muda mrefu sana, nanyi. Lakini kumbukeni, mfalme alituma na akaandaa chakula cha jioni. Alichinja fahali wake wote, na—na kuwaandaa walio wanono na kila kitu, akaandaa chakula kikuu sana cha jioni. Naye akatuma, na akawaalika wengi waje.

Mmoja alisema, "Vema, unajua, hata hivyo, mimi ni mfuasi wa *hili*." "Nami nina jambo *hili*." "Sina budi kwenda shambani kwangu." Na mmoja alifanya mambo mengi. Naye akatuma tena, nao wakawatenda mabaya. Na hatimaye … Hicho kilikuwa ni kizazi cha Wayahudi, ambacho Yesu alikuwa akizungumza nacho. Walikuwa na jambo lingine la kufanya.

Ndipo, hatimaye, akatuma, "Na kusema … Nendeni. Msininii tu … Washurutisheni tu. Nendeni barabarani na kwenye barabara kuu, na kila mahali, na kuwashurutisha waingie." Na baada ya hayo, akadhamiria ya kwamba nyumba yake ilikuwa … Karamu yake ya arusi ilikuwa inaenda kuandaliwa. Kutakuwa na wageni kule.

Ndipo akamkuta mtu mle ndani asiyevaa vazi la arusi. Alitaka kushikilia lile koti la kale. Basi angalia yale aliyosema. "Rafiki, baada ya kukualika kwenye karamu yangu ya arusi, nami nilikualika na kukupa mwaliko wa kuja!"

80 Na kama uliwahi kuwa katika nchi za Mashariki, ambalo nililihubiri mara nyingi, hiyo karamu ya arusi ingali inaendelezwa tu jinsi ilivyokuwa ikifanyika. Bwana arusi, ambaye, wote, yeye ana wageni wengi sana ambao atakuwa nao. Labda, Ndugu Kopp, labda umeitazama huko India. Unaona? Wana wageni

wengi sana ambao atawaalika; tuseme atawaalika wageni thelathini.

Sasa, bwana arusi hana budi kutoa mavazi. Hana budi kuyatoa, kwa hiyo kuna mtu anayesimama mlangoni. Nawe unakuja na mwaliko wako. Yeye huchunguza mwaliko wako na kukuvalisha vazi, joho. Kwamba, baadhi yao ni matajiri, na wengine wao ni maskini, na wengine wao ni tofauti, lakini wote wanafanana wanapovalia mavazi haya. Wote wanafanana.

Nanyi nyote mnapaswa kufanana. Hamtakuwa, tuseme, "Mimi ni Mmethodisti *hapa*. Mimi ni Mpresbiteri *hapa*." Loo, la. Hutaingia, kwanza. Unaona?

Huna budi kupitia Mlangoni. Yesu alisema, "Mimi Ndimi Mlango wa zizi la kondoo."

"Mimi ni Mpentekoste. Mimi ni *hili*. Mimi ni *lile*." Hilo halimaanishi kitu.

Unakuja kwa Mlango huo. Na kama ukija kupitia Mlango huo, unapata vazi.

81 Na mtu huyu, wakati aliposema, "Uliingiaje humu, rafiki?" Unaona?

Ilionyesha alikuja kupitia njia nyingine, na alikuja kupitia dirishani, akaingia kwa njia ya hadaa, lakini si kupitia mlangoni; si kupitia ule Mlango, jinsiambavyo Yesu alikuja, kwa kujitoa dhabihu Mwenyewe; kumtolea Mungu yote uliyo nayo, na kutembea kwenda Kalvari na kusulubiwa pamoja Naye. Na kufufuka tena, upate kuvaa vazi Lake la dhabihu na mauti kwa mambo ya ulimwengu.

"Ukiipenda dunia, ama mambo ya ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Unaona? Kama ungali unaupenda ulimwengu, unataka kutenda kama ulimwengu, na kutenda kama ulimwengu; unajaribu … unaninii … Huku, wewe uko kanisani, lakini ni gugu shambani pamoja na ngano; unapiga kelele pamoja na hao wengine, unafurahi pamoja na hao wengine. Baraka zote za kiroho ziko juu yako.

Unasema, "Vema, natabiri." Vivyo hivyo na Kayafa pia. Vivyo hivyo na Balaamu. Hilo halihusiani …

82 "Nina ubatizo, Roho Mtakatifu." Hilo bado halihusiani nalo. Hiyo ni karama ya muda tu kwako.

Karama halisi ni nafsi yako kule ndani, unaona, hiyo iliyozaliwa na Mungu, na hiyo inatawala kitu hicho chote kwa Neno la Mungu na mapenzi ya Mungu. Na hapo unakua, unaona, ndipo wewe ni mwana na binti wa Mungu. Wewe ni mtoto wa Mungu. Na mambo haya, unapokuwa ukija … Kama vile mama, sasa uko katika tumbo la dunia, ukijaribu kutoka. Wewe ni mwana wa Mungu, ukija, na unaona Neno likisema, "Inanipasa kufanya jambo *hili*. Ninapaswa kuzaliwa mara ya pili."

"Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa." Hilo halimaanishi kitu. Unaona?

"Mimi ni Mmethodisti; mama yangu." Hilo ni zuri kwa mama yako.

"Vema, jamani, mimi ni Mpentekoste. Mimi ni mfuasi." Kwamba, kama hulilingani hilo Neno hilo, kuna kasoro fulani. Unaona? Halafu, unaona, baba yako halisi si Mungu. Unaona? Kwa sababu, huo mwanzo halisi katika nafsi yako, kabla hata hapajakuwako na roho, ilikuwa ni nafsi yako. Nafsi hiyo haikutokana na Mungu, basi haikuwa ni seli hai ya uzazi ya Mungu, kwanza. Umedanganywa. Uko katika ardhi ya magugu na unashuhudia ulimwengu wa magugu yanayotokeza. Kutenda kama ulimwengu, kuupenda ulimwengu, ni kwa sababu kumpenda Mungu hakumo ndani yako.

83 Na sasa kutakuwako na wapakwa mafuta wa uongo katika siku za mwisho, si Yesu wa uongo. Wasingevumilia jambo hilo. Lakini, "wa uongo," waliopakwa mafuta. Wamepakwa mafuta, naam, bwana, bali wao ni wapinga Kristo. Wamepakwa mafuta kwa Roho, kufanya ishara na maajabu ambayo Kristo alifanya, lakini hawatalifuata Neno Lake. Unaona?

"Wengi watakuja Kwangu, Siku hiyo, na kusema, 'Bwana, je, mimi sikutabiri, na kutoa mapepo, katika Jina Lako?'"

Yeye atasema, "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Sikuwajua ninyi kamwe."

"Nilikuwa Mpentekoste, Bwana. Utukufu kwa Mungu! Nikapaza sauti. Nilinena kwa lugha. Nami nikaweka mikono yangu juu ya wagonjwa, na kuwaponya, nikatoa mapepo."

"Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu. Sikuwajua kamwe."

84 Mnaona ninalomaanisha? Loo, enyi watoto wadogo, mnajisikia haja ya vitamini hiyo usiku huu, kitu kama hicho? Kuna mwili unaongojea kule ng'ambo. Kuna mwili unaongojea kupokelewa. Enyi watu, msidanganyike. Msidanganyike. Ibilisi ni mdanganyifu. Hata va—vazi la arusi, huna budi kulivalia. Lazima iwe hivyo.

Sasa tuko kwenye wakati wa jioni. Mwili wa duniani sasa uko tayari kuharibiwa, nasi tunajiandaa kuingia katika ule wa Kimbinguni. Nasi sasa tunahisi wito wa ajabu, wa Mungu, kwenda kwenye Edeni hii kuu. Na kabla hatujazaliwa hapa, miili yetu midogo ililia kitu fulani ambacho—ambacho kilipaswa

kutolewa, la sivyo tungekuwa watoto wanaoteseka hapa kama hatukukipata. Mungu hana mateso huko juu. Wao, kila mmoja wao, wamejipanga kikamilifu, Bibi -arusi hasa kama Bwana Arusi alivyokuwa, Neno lililodhihirishwa katika majira Yake. Mungu tujalie, usiku huu, watoto, kila mmoja wenu! Kuna Mbingu ya kwenda. Kuna kuzimu ya kuepuka.

85 Sasa, wengi wenu mnajua kwamba Bwana amenipa maono, maelfu ya hayo. Jambo kuu sana kuliko yote … Nilikuwa nikihofu mauti. Yapata miaka mitatu iliyopita, mmewaona Wanaume Wakristo Wafanyabiashara, *Ng'ambo Ya Pazia La Wakati*. Natambua huenda nisiishi kumaliza usiku huu. Huenda nisiwaone tena katika maisha yangu hapa, lakini hili ni kweli. Si—sijui kama ningeliita hili ono, ama lilikuwa kitu gani.

Asubuhi moja, hivi majuzi, nilikuwa … Nilikuwa ndio tu nimeamka. Nilikuwa nimekuja kutoka kwenye mikutano. Na mke wangu alikuwa amelala pale, usingizini. Nikasema, "Mpenzi, umeamka?" Alikuwa bado amelala. Nilijua ilitupasa tuamke, ili kuwapeleka watoto shuleni.

Nami nikaweka mikono yangu juu, namna hii, na nikasema, "Vema, aisee, Bill Branham, unajua umepita miaka hamsini? Wewe, kama utafanya jambo fulani kwa ajili ya Bwana, ni bora uharakishe, maana huna wakati mwingi zaidi." Nikawaza, "Jamani, natumaini ya kwamba ninaweza kuishi nipate kuona Kuja kwa Bwana Yesu."

Daima nilikuwa na jambo hilo moyoni mwangu, kwamba-kwamba tunapokufa, ningeona, kama, ndugu *hapa*. Ningesema … "Naam, ulihubiri kanisani kwangu, usiku mmoja kule duniani, Ndugu Branham." Lakini, yeye—yeye ni roho, nisingeweza kumpa mkono, kwa sababu mkono wake uko kule kaburini, umeoza, unaona; wangu, pia. Nilikuwa kwa namna fulani nikiwazia jambo hilo.

86 Lakini asubuhi hiyo, wakati, nilisikia kitu Fulani kikinijia. Nami nikawaza … Kwa kawaida, kama vile ono linavyokuja. Nami nikaangalia, nami ni—nikaangalia. Nikawaza, "Jamani! Ni kitu gani hiki?" Nami nikaangalia, vilima vikubwa vya kijani kibichi. Na wasichana walikuwa wakija kutokea kila mahali, kwa makumi elfu, na mamia ya maelfu. Nao wote walikuwa wakija, nywele ndefu zikining'inia mgongoni mwao, wamevaa mavazi meupe, bila viatu, wakipiga makelele, wakishangilia, "Ndugu yetu!"

Ni—nikawaza, "Sasa, hili ni la ajabu." Nikageuka nyuma na kuangalia. Na hapo nililala papo hapo, na huyo hapo mke wangu, amelala pale kitandani. Nami nikasema, "Sasa, unajua nini? Nilikufa." Nikasema, "Hilo, hilo ndilo lililotokea. Ni—nimekufa." Nami nikasema, "Huenda nilipata ugonjwa wa moyo, ama kitu fulani. Nimekufa. Huo hapo mwili wangu umelala." Nilikuwa tu nimelala pale huku nimerudisha mikono yangu nyuma, namna *hiyo*, nimekauka tu. Nikawaza, "Huo hauko futi ishirini kutokea kwangu." Nami nilikuwa pale, nikiangalia. Nikawaza, "Hiyo ni … Yule pale mke wangu. Kuna, kuna kila kitu. Kuna shati langu lililoning'inia pale kwenye kile kizingiti cha kitanda." Nami nikawaza, "Huyu mimi hapa."

87 Nikaangalia huku na huko tena, na wanawake hawa wote walikuwa wakija. Nao walikuwa … Nikaangalia, wakija upande *huu*, na pale wanakuja ndugu zangu. Loo! Wao ni halisi. Wote walionekana kuwa vijana. Walikuwa wakipiga makelele, "Ndugu yetu wa thamani!" Loo, sikujua la kuwazia.

Nikawaza, "Hili ni jambo la ajabu." Nikaangalia nyuma, nami sikuwa mzee. Nilikuwa kijana. Nikawaza, "Hili ni jambo la ajabu." Nikawaza, "Je! Hili ni ono?" Ningeng'ata kidole changu. Na nikawaza, "La. Si aina ya ono ambalo nimekuwa nalo."

Ndipo, hapo, kitu Fulani kikaanza kuzungumza na mimi *hapa* juu, na kusema, "Umeingia pamoja na watu wako."

Nikawaza, "Pamoja na watu wangu? Je! Hawa wote ni akina Branham?"

Ikasema, "Hao ni waongofu wako kwa Kristo." Na wanawake hawa …

Unajua daima nimewaziwa, kwa sababu wao wangaliniita "mchukia wanawake," bali sivyo. Unaona? Maana, naamini … Si—si—sipendi uzinzi, tabia mbaya. Nawapenda dada halisi, wa kweli wa Kristo. Kama wako hivyo, sawa.

88 Nilikuwa na makovu nilipokuwa mtoto mdogo. Najua mambo yaliyotokea ambayo kwa namna fulani yamenigeuza mwelekeo wangu namna hiyo. Lakini hilo—yote yalikuwa ni Mungu, akifanya, akinifinyanga kwa ajili ya saa hii. Unaona?

Nafikiri dada halisi, wa kweli, hakuna kitu kilicho kizuri zaidi. Kama Mungu angeweza kumpa mwanamume kitu cho chote kilicho bora kuliko wokovu, Yeye angempa mke. Unaona? Na kwa hiyo, basi, kama angaliweza kumpa kitu cho chote kilicho bora zaidi, angalifanya hivyo. Na halafu basi kuona baadhi yao wakigeuka na hata hawatendi kama mke, wasio waaminifu kwenye nadhiri zao za ndoa, na waume zao vivyo hivyo. Kumbuka, umefungwa maadam uko hai, mmoja kwa mwingine. "Kile Mungu anachounganisha duniani, kimeunganishwa Mbinguni pia." Unaona?

89 Na kwa hiyo basi ni—niliona jambo hilo. Na wanawake hawa walikimbia na walikuwa wakinikumbatia

kwa mikono yao, na kunikumbatia, na kuniita, "Ndugu!" Sasa, wao walikuwa ni wanawake, lakini kamwe hakuwezi kuwa na dhambi mahali hapo. Unaona? Walikuwa ni wanawake. Lakini, unaona, kilichotufanya sasa, mwanamke mwenye te—tezi, tezi ya kike, na mwanamume mwenye tezi ya kiume, ni kwa ajili ya kuinua watoto. Hapo hakutakuwako. Wote watakuwa na tezi moja, bali bado watakuwa katika umbo lao. Ile sura ya duniani waliyokuwa nayo hapa itakuwa kule, lakini kamwe hakutaweza kuwako na dhambi. Ninyi nyote mmefanana. Hakutakuwa na watoto watakaozaliwa kule. Unaona? Hiyo ni kweli. Yote yatakuwa hivyo. Na kwa hivyo nikaangalia, na hawa wanawake.

90 Nao wakanichukua juu. Hawa ndugu wakaniweka mahali fulani. Nikasema, "Kwa nini mnafanya jambo hili?"

Yeye akasema, "Duniani ulikuwa kiongozi." Kisha akasema—na kusema, "Wewe … Hawa ndio wale watu."

Na kulikuwa na mwanamke fulani aliyejitokeza. Akasema, "Ndugu yetu wa thamani." Mwanamke mzuri sana!

Wakati alipopita pale, Sauti hii ilinyamaza, ikasema, "Hivi humkumbuki?"

Nikasema, "La."

Ikasema, "Ulimwongoza kwa Kristo alipokuwa amepita umri wa miaka tisini. Unaona? Huwezi kuona ni kwa nini anasema 'ndugu wa thamani'?"

Nikasema, "Vema, una—unaenda …"

Kasema, "La. Tunangojea hapa."

Nikasema, "Vema, kama nimeaga dunia, nataka kumwona Yesu."

Ikasema, "Huwezi kumwona sasa. Haya ni Maandiko, yalisema, 'Nafsi zilizo chini ya madhabahu.' Yeye yuko juu kidogo tu. Siku moja Yeye atarudi. Tunarudi duniani. Hatula wala kunywa hapa."

91 Nikasema, "Unamaanisha niliogopa jambo hili? Mbona, hii …"

Hakuna neno la kunena jambo hilo, enyi marafiki. "Ni pakamilifu," lisi—lisingepagusa, "pa heri." Hakuna msamiati wa Kiingereza ninaoujua, hakuna neno hata kidogo, ambalo ungeweza kuelezea ni nini. Ni zaidi ya chochote nijuacho. Huyo hapo. Hakukuwa na magonjwa, hakuna huzuni. Usingeweza kufa. Usingeweza kutenda dhambi. Palikuwa ni pakamilifu tu, pakamilifu tu. Enyi marafiki, haiwapasi, haiwapasi kupakosa. Kumbukeni.

Na nilipokuwa mvulana mdogo, niliona ono la kuzimu, kama mvulana mdogo. Nanyi mnajua jinsi mabibi, leo hii, ama wanawake (akina bibiye wasingefanya jambo kama hilo), kupaka rangi macho yao kama mbwa mwitu, ama kitu fulani kama hicho, vitu hivyo vya bluu chini ya jicho lao. Niliona kitu hicho. Nilikuwa nikizama. Kama mvulana mdogo, nilikuwa nimepigwa risasi, nami nilikuwa nimelala, nikifa hospitalini. Nami daima nilijua kulikuwa na Mungu.

Nakumbuka maombi ya kwanza niliyowahi kuomba. Jambo pekee ningeweza kusema … Si—sijawahi kusema jambo hili hapo awali. Najisikia tu nilisimulie sasa hivi. Nilikuwa nimepigwa risasi, nimelala pale, nikifa shambani. Na ombi pekee nililoweza kuwa nalo kwa Mungu, nilisema, "Unajua, Bwana, kamwe sikufanya uzinzi." Unaona? Kama mvulana mdogo, mwenye umri wa karibu miaka kumi na mitano, nilijaribu kuishi msafi. Nami nikasema, "Nimeishi msafi." Na hilo tu ndilo niliweza kusema. Hiao ndiyo matendo mema pekee niliyoweza kumpa Yeye.

92 Na halafu nikiwa nimelala pale, basi, wakati daktari alipoondoka nilikokuwa, nami nikajisikia nikizama katika Umilele wenye giza, ilivyoonekana. Nikamlilia baba, "Loo, baba, nisaidie." Hapakuwepo na baba kule. "Mama, nisaidie." Hakukuwako na mama kule. "Mungu, nisaidie." Hakukuweko na Mungu kule. Ilikuwa tu ni jinamizi lisilo na mwisho, la kutisha, loo. Kuzimu kunakowaka moto mkubwa kungekuwa ni raha, kule kuwa kando yake. Na nikiwa naangukia kule, nikawaza, "Loo, jamani!" Kuvingirika na kuvingirika, namna hii. Nilifikia mahali, moshi, na giza, na mgonjwa. Na, loo, kujisikia kwa namna hiyo! Ilikuwa ni mauti kwangu.

Nami niliweza kuwaona hao wanawake wakinijia, wakiwa na namna hiyo ya macho yaliyopakwa rangi namna hiyo. Sasa kumbukeni, hilo limekuwa ni miaka arobaini na mitano iliyopita, takriban miaka arobaini iliyopita, hata hivyo. Wakienda, walikuwa wanaenda, "Oooh! Oooh! Oooh!"

Nikasema, "Je! Nitakuwa huko milele?"

"Daima."

Nikasema, "Ee Mungu, kama utaniruhusu nitoke hapa, si—si—sitakuonea aibu tena. Sitakuonea aibu

kamwe. Mungu, tafadhali nipe nafasi."

Jambo la kwanza unajua, nilijisikia nikirudi. Naye daktari akashtuka, maana moyo wangu ulikuwa ukipiga tu mara kumi na saba kwa dakikao. Tayari nimetoka damu yangu yote na kila kitu, nilikuwa nimelala katika damu yangu mwenyewe. Nami nimeshangaa, hivi siku moja jambo hilo lingetokea?

93 Yapata miaka miwili iliyopita, nilipohamia Tucson, nilikuwa pamoja na mke wangu huko J. C. Penney. Nilikuwa nimeketi pale namna *hiyo*, huku nimeinamisha kichwa changu, nikingojea. Maana, mnajua jinsi ambavyo, akina bibiye, wanazunguka madukani kwa muda mrefu. Nami nilikuwa—nilikuwa nimeketi pale, nimeinamisha kichwa changu namna *hii*. Na kipandio kilikuwa kikija juu. Na hawa hapa wanakuja baadhi ya hao wanawake, wakiwa na nywele zilizonyolewa mtindo wa kichwa maji, uajua, kama wanavyofanya, namna *hiyo*. Wakija na hayo macho yaliyoonekana kupakwa rangi namna hiyo. Nao walikuwa wakizungumza Kihispania. Na hilo ndilo jambo lenyewe. Lote (lile ono) lilitokea tena. Hilo hapo, "Oooh! Oooh!"

Ndugu, dada, hebu niwaambie jambo fulani. Huenda likaonekana ni jambo la kuchekesha sasa, bali mara unapofika kule. Ni jambo zito. Usiiendee njia hiyo kamwe.

94 Mimi, kama mzee, mhudumu, nimehubiri kote ulimwenguni, nina mamilioni ya marafiki, lakini najua sina budi kusimama nanyi huko ng'ambo. Ondokeni kwenye mambo ya ulimwengu. Na kama kuna kitu fulani ndani yako, kwamba ungali unataka kutenda jinsi unavyotenda, kama una mambo ya ulimwengu ndani yako, kumbuka, wewe si wa Mungu. Wewe ni mfuasi tu wa kanisa, mpaka wito huo; hicho kilindi, kikiita Kilindi. Unaona?

Kama vile, kabla hapajakuwa na pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi kuwepo na maji kwa ajili yake kuogelea humo, kwanza, la sivyo asingekuwa na pezi kamwe.

Kabla hakujakuwako na m—mti wa kuota duniani, ilibidi kuwe na ardhi, la sivyo kusingekuwako na mti wa kukua ndani yake. Kusingekuwa na sababu ya mti huo, na kuufanya uwe pamoja nayo.

95 Kabla ya kuwepo uumbaji, hapana budi pawe na Muumba. "Heri wenye njaa na kiu ya haki." Unaona? Kuna kitu fulani ndani yetu. Uliinua mkono wako muda mfupi uliopita, "Namhitaji Mungu zaidi." Unaona? Kuna kitu fulani kinachohitaji.

Na kama ukiupenda ulimwengu, ukiiendea njia hiyo, mambo ya ulimwengu, utaiendea njia ya ulimwengu, nawe utaanguka. Unaona? Tokeni. Ninyi ni wana na binti za Mfalme, yule Mfalme. Iweni bibiye na muungwana. Tembeeni kama Wakristo. Ishini kama Wakristo. Tendeni kama Wakristo. Kumbukeni, nitakutana nanyi kwenye Kiti cha Hukumu pamoja na matamshi haya. Unaona?

Angalia katika kioo chako cha kutazamia, usiku huu, uone. "Ninaelekea upande gani? Je! Yesu ananiandalia mahali, mwili? Mwili huo ni mkamilifu. Mwili huo unatembea kwa utaratibu. Ni mwana ama binti mbele za Mungu. Nami nina utungu wa kuzaa ndani *humu*, kuzaliwa katika mwili huo kule. Kama ningali ninaupenda ulimwengu, inanionyesha kwamba (mimi siko) sina mwili kule. Mimi ni mfuasi tu wa kanisa. Mimi sikuwa ni seli zazi ya Mungu. Mimi siyo seli zazi. Yeye si Baba yangu."

96 Yeye alisema, "Kama hamwezi kustahimili kurudiwa," hayo ndiyo mnayoyapata sasa, "basi ninyi ni wana haramu, wala si watoto wa Mungu." Hiyo si ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Sawa." - Mh.] Je! Biblia inasema hivyo? ["Amina."]

Kama huwezi kustahimili kurudiwa na Mungu, wakati unapoona Maandiko yakikuweka sawa, nawe unasema, "Loo, sitaki kusikia mambo hayo. Mimi ni—mimi ni Mkristo. Ninafanya ninii …" Vema. Endelea. Unaona? Huo ni ushahid mmoja wa hakika kwamba wewe si mwana wa Mungu.

Lakini mtoto halisi wa Mungu ana njaa na kiu. Kwa nini? Kama kuna kitu fulani moyoni mwako, kinachokwambia unakitaka hicho, na kinahitaji humo, inaonyesha kuna kitu fulani kinachodundadunda, kikijaribu kukuvuta kule. Kuna mwili kule, ambao *huu* ni mfano wa hapa. Unautumia huu kwa ajili gani, kumtukuza ibilisi na ulimwengu, na mitindo na kadhalika? Je! Unaangalia Mbinguni, kuna kitu fulani kule juu, unamtukuza Mungu kwa maisha yako?

> *Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningewaambia*. Nami nitaenda na *kuwaandalia mahali.*
>
> *… nitakuja tena, kuwakaribisha kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo.*

*Mambo Yatakayokuwako*. Mambo haya yaliyoko sasa, ni uwezekano tu, yakitaka mambo yatakayokuwako.

Hebu na tuombe.

97 Wazeni kwa uzito. Je, mtafanya hivyo, enyi wapenzi marafiki Wakristo? Wazeni kwa makini sana, kwa

muda kidogo tu. Hebu na tuwe kimya kabisa kwa muda kidogo tu. Hebu Roho Mtakatifu anene.

Sasa, Bwana Yesu alinituma kwenu Wapentekoste, muda mrefu uliopita. Huyu hapa mmoja wa wavulana wenu ambaye amekuja kuwa mchungaji wenu, kasema, "Alitokana na hii huduma." Yeye alimwona Bwana Yesu akiyafumbua macho yaliyopofushwa; "kufanya," yeye alisema, "vichwa maji vikome mara moja." Ningali nina ibada za uponyaji. Lakini natambua kwamba nimewaombea watu wengi waliokuwa wagonjwa sana. Waliponywa. Bwana alijibu maombi, na kuwaponya wagonjwa. Lakini, unajua, baadhi ya hao watu, walioponywa, tayari wamekufa. Na haidhuru wewe ni mgonjwa jinsi gani, kama umeponywa, utakufa, hata hivyo.

Lakini hiyo nafsi, ndugu yangu wa thamani, hiyo nafsi, dada yangu wa thamani, hivi hutaiwazia sasa? Hiyo ni ya Milele. Kama upendo huo wa Mungu haumo ndani mle, hakuna kitu kinachovuta, je! Huwezi kumwomba Mungu, "Ewe Mungu, nianzishe tena, upya, usiku huu. Nakupenda, Bwana. Nataka kukupenda Wewe. Na kitu fulani moyoni mwangu kinaniambia kwamba sina budi kuishi karibu zaidi na Wewe. Nataka kuja, sasa hivi, Bwana, na kufanya jambo hilo"? Kama mtu huyo au watu hao wako katika jengo hili au nje ya jengo hili, nawasihi, kama mtumishi wa Kristo, katika Jina la Yesu Kristo, mtaninii tu, huku umeinamisha kichwa chako, umwinulie Mungu mkono wako juu na useme hili, "Mungu, nivute karibu zaidi, karibu zaidi, Mungu mpenzi. Nataka kuendana na kila kitu ulicho nacho katika Neno Lako"? Inueni mikono yenu juu. Sasa iweni waaminifu kabisa. Wazeni tu.

98 Sasa, wao wanasema, "Loo, nimefanya jambo *hili*. Mimi, nimepaza sauti, Roho. Nimenena kwa lugha. Lakini, angalia, kuna kitu kinachokosekana maishani mwangu. Naangalia katika kioo cha Neno la Mungu, najua kuna kitu fulani. Naenda kanisani, lakini siko vile ninavyopaswa kuwa." Unaona? Hiyo inaonyesha ya kwamba, kitu fulani.

Sasa, kama unaweza kujiangalia mwenyewe na uone kwamba hujalilingana Neno la Mungu, na hakuna kitu humo ndani kitakachokusababisha kuinua mkono wako juu, basi unajua kuna kasoro fulani. Unayo. Kuna … Mama alizoea kusema, "Huwezi kupata damu kutoka kwenye tanipu, kwa sababu hakuna damu ndani yake." Unaona? Wazia jambo hilo, kwa makini hasa. Hii huenda ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho. Mikono thelathini, arobaini imeinuliwa juu, kundi hili dogo hapa, hata kwa makasisi.

99 Iweni tu na kicho sana kwa muda kidogo tu. Sasa hebu wazeni kwa makini sana. "Mungu mpenzi, huenda nikauawa, usiku huu, katika ajali. Huenda nikafa kwa ugonjwa wa moyo. Moja ya asubuhi hizi, huenda nikamwita daktari, naye akaja, na mapigo yangu ya moyo yanagonga mkono wangu wa shati; Nimeondoka. Ninakandamiza shavu langu kwenye mito, nikiita, 'Ewe Mungu! Ewe Mungu! Ewe Mungu! '" Unaona? Moyo huo unapiga pigo lake la mwisho. Unakuja kwenye ule Mlango mkuu. Kamwe hutatoka isipokuwa uwe umezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Kamwe hutatoka isipokuwa kuwe na kitu fulani ndani yako, baada ya kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, ukiona njaa na kiu ya kuendelea pamoja na Mungu. Lazima iwe hivyo. Unaona? Wewe ni mtoto duniani, katika tumbo la dunia, ungali unangojea kuzaliwa katika Ufalme wa Mungu, ambako Yeye ameenda kukuandalia mwili mwingine, huo ni mwili mkamilifu.

Sasa hebu wazeni kwa kilindi hasa, na hebu tuombe pamoja.

100 Mungu mpenzi, kama ninavyojua ya kwamba haya yameandikwa kwenye kurasa za Kitabu, ile Kumbukumbu kuu! Tumekosea katika sayansi, Bwana, vya kutosha kutuamsha, kwa mambo halisi kujua kwamba kila hatua tunayochukua inazunguka na kuzunguka ulimwenguni, wakati ule ule tunaposogea. Tumejua hayo kupitia kwenye televisheni. Tunatambua, Baba, kwamba hiyo televisheni haitengenezi picha, inaelekeza tu mi—mitetemo ndani ya chubu inayotengeneza picha. Hata rangi ya nguo ambazo tumevaa, zinaonyesha kupitia mawimbi ya etha ya hewa, mitetemo hiyo kote ulimwenguni. Basi vipi dada zetu waliovaa hizo nguo, wakitenda hivyo, wala hata hawana njaa; nyuso zilizopakwa rangi, kukata nywele?

Wahudumu ambao wangeenda kwenye theolojia, seminari fulani, "Na kuchukua mambo ya neno la mwanadamu, ambaye anafanya, kwa njia ya mapokeo yao, wanazifanya amri za Mungu zisiwe na nguvu juu ya watu, kwa njia ya mapokeo yao," wakisema wanapaswa kuwa wafuasi wa kanisa, na ni hivyo tu.

Ewe Mungu, je! Wanatambua kwamba kila neno tunalosema, limethibitishwa kisayansi, liko kwenye kumbukumbu? Na inaanza tunapoanza kuishi katika dunia hii. Inaishia tunapokufa, na inawekwa katika albamu ya Mungu, ipate kuchezwa tena kwenye Hukumu.

Tutaepukaje jambo hilo, hukumu ya Mungu, kama jambo hilo limefanywa wazi sana mbele zetu na hata hivyo tunalikataa?

Ee Mungu mpenzi, Maneno haya hayafi kamwe. Yanaendelea na kuendelea. Hiyo kumbukumbu itachezwa kwenye Siku ya Hukumu. Umeona hiyo mikono iliyoinuliwa juu, Baba. Itakuwa pale pale kwenye Siku ya Hukumu. Pia, yale mioyo yao ilikuwa ikiwazia, yatakuwako pale kwenye ile Siku ya Hukumu.

101 Sasa, Baba, Mungu, nakuomba, kama mtumishi Wako, naomba kwamba utaondoa uovu wote kwa

watu Wako. *Uovu*: jambo fulani ambalo tunajua tunapaswa kufanya, na hatulifanyi. Daudi alisema, "Nikiwaza uovu moyoni mwangu, Mungu hatajibu maombi yangu." Naomba, Mungu, kwamba utauchukua uovu wetu, maana Neno ndilo kioo Chako cha kujiangalia ambacho kinatuonyesha jinsi tulivyopungukiwa kuwa wana na binti za Mfalme. Baba, naomba ya kwamba utalifanya hilo, usiku huu.

Na ufanye hiyo kuwa madhabahu, maana madhabahu imejaa watu. Na ufanye hiyo kuwa madhabahu, hapo kwenye kiti ambapo wameketi, ufanye huo moyo wao kuwa madhabahu. Jalia ulimwengu ujitenge na kila ndugu, dada hapa. Na jalia hiyo seli zazi ndogo ya Uzima, jeni ya Mungu ambayo ndiyo kwanza tuizungumzie, ile sifa iliyoshuka kutoka kwa Mungu, na imedhihirishwa hapa imheshimu na kumtukuza Mungu. Mungu, ondoa ulimwengu kutoka humo.

Hao wengine, siwezi kuomba, Bwana, kwa sababu "ugonjwa huo ni wa mauti," na hakuna kitu hapo kinachowafanya wasogee. Lakini wale ambao wanaweza kusogea, na wanajua kwamba ni makosa, isafishe mioyo yao na nafsi zao, usiku huu, Baba. Na jalia wajazwe kwa Roho Wako, watembee katika Nuru Yako.

102 Mbariki mchungaji huyu mpendwa, kijana, mwenye afya, mwenye nguvu hapa, Bwana. Huyu mvulana, alishawishiwa, alisema, kwa yale aliyokuona ukifanya. Huyu mvulana mzuri, Ewe Mungu, iwashe moto nafsi yake. Tujalie, Bwana. Jalia awe mchungaji wa kweli, daima, wakati wote, apate kulilisha kundi ambalo Roho Mtakatifu amemfanya msimamizi juu yake. Tujalie hilo, Bwana. Jalia asigeuke kulia wala kushoto, hakuna njia kwa ajili ya kanuni yoyote ya imani, hakuna kitu kingine ila Neno la Mungu lisiloghoshiwa likitoka kinywani mwake, na Hilo pekee. Mbariki, Mungu, yeye na wapenzi wake, na kanisa lake dogo hapa. Uwe pamoja nao wote, Baba.

Nakabidhi hili Kwako, Baba. Mbegu imepandwa. Jalia Hiyo ianguke juu ya hiyo mbegu iliyochaguliwa kwa ajili ya Uzima, na kukua, wawe Wakristo wakuu, wenye nguvu kwa ajili ya kusanyiko hili hapa, na makusanyiko mengine wanakotokea. Tujalie hilo, Bwana. Ninayakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

Na, Baba, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa."

103 Nilimwona maskini mwanamke mwenye wasiwasi, muda mfupi uliopita, akipitia mlangoni. Na, Ewe Mungu, katika familia yake mwenyewe, ni mambo makuu jinsi gani yamefanywa, jinsi ambavyo umejidhihirisha Mwenyewe! Naomba, Mungu, kwa ajili ya mwanamke huyo. Ondoa hayo yote yaliyopita, ya maisha, Bwana, na umponye usiku huu. Utafanya hivyo, Bwana? Mchukue Kwako.

Unaona jambo hilo, watoto wadogo wakiwa wameketi hapa, Bwana, wakihitaji uponyaji, wengine. Naomba ya kwamba utawaponya, Baba. Tujalie hilo. Jalia nguvu Zako kuu za uponyaji zije na zituponye, nafsi na mwili pia.

104 Na sasa, kwenu ninyi mlio kanisani hapa, ama nje, mnaohitaji uponyaji, nataka uinue mkono wako juu, useme, "Nahitaji uponyaji, Ndugu Branham." Inaonekana kama kila mtu anahitaji. Vema. Je! Mtaniamini mimi kuwa mtumishi wa Kristo? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Basi, nawatakeni mwekeane mikono. Wekeaneni tu mikono yenu. Ninyi mlioinua mikono yenu, mlio ndani au nje, inuaeni mikono yenu juu, ya kwamba ninyi mlikuwa mwaamini katika Mungu.

Yesu Kristo alisema, agizo Lake la mwisho kwa Kanisa, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Yeye aaminiye … Yeye aaminiye na kubatizwa ataokoka. Yeye asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitawafuata hao waaminio; katika Jina Langu watatoa mapepo; watanena kwa lugha mpya; kama wakishika nyoka au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; lakini, na kama wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Sasa, Yesu alisema jambo hilo. Kumbukeni, Yeye alisema hayo. Hayo hayana budi kutimia. Asingesema hilo isipokuwa kuwe na mtu fulani angeweza kulishika hilo Neno.

105 Kama tu vile tumbo la uzazi la Mariamu lingeweza kushika ile seli zazi, "Bikira atachukua mimba." Kama vile mtende ungeweza kuumbwa, mwaloni kwenye kilima, Neno Lake lilifanya hivyo.

Neno Lake linaweza kuingia moyoni mwako sasa hivi. "Mimi ni mwamini, Bwana. Huyu mwanamume ama mwanamke niliyemwekea mikono, wanateseka. Mimi sijiombei mwenyewe. Kwa sababu, wao wananiombea. Ninamwombea mwanamke huyu, ama kwa ajili yake mwanamume hyu. Na, Ewe Mungu, mponye mwanamume huyu, mponye mwanamke huyu. Nami ni mwamini, na sasa tumekusanyika. Tumefundishwa tu ya kwamba tulikuwa pamoja na Kristo wakati alipotembea duniani, kwa kuwa sisi ni sehemu ya Neno Lake. Tuliteseka pamoja Naye. Tulitokwa na damu pamoja Naye. Tulikufa pamoja Naye. Tulizikwa pamoja Naye. Tumefufuka pamoja Naye, nasi tunaketi pamoja katika sehemu za Kimbinguni katika Kristo Yesu. Yule Mfalme mkuu akiwa ameketi hapa katikati yetu, nami ni mwana ama binti wa huyu Mfalme. Nami nimeweka mkono wangu juu ya mwana ama binti wa Mfalme, anayeniombea, nami ninawaombea. Sasa, Bwana, jibu ombi langu, na umponye huyu mwana wa Mungu ama huyu binti wa Mungu."

Pamoja, hebu tuombeane sisi kwa sisi.

106 Bwana Yesu, tunakuja kwa unyenyekevu, tukikiri makosa yetu. Tunakuja, tukikiri ya kwamba tunastahili magonjwa na mauti, na huzuni, lakini tunakubali upatanisho Wako kwa ajili ya dhambi zetu na magonjwa yetu. Na, usiku huu, hawa wana na binti za Mungu, wakiwa wameketi hapa, wanasikia masahihisho ya Neno, na wakiinua mikono yao, na wakitaka kuwa karibu zaidi. Wanawekeana mikono sasa kwa sababu wanaamini Neno Lako kuwa ni kweli. Wanaamini ya kwamba sasa tumefufuka pamoja na Kristo, wakiwa wameketi katika sehemu za Kimbinguni pamoja Naye. Waliwekeana mikono, wakiombeana.

Ulisema, "Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa, na Mungu atamwinua; na kama amefanya dhambi yo yote, atasamehewa. Mkiungamiana makosa yenu ninyi kwa ninyi, mkiombeana, mpate kuponywa. Kwa maana maombi yenye bidii ya mwenye haki yana nguvu nyingi." Ewe Mungu wa Milele, sikia maombi ya watumishi Wako.

Na sasa, imeandikwa tena, "Kama watu, walioitwa kwa Jina Langu, watakusanyika pamoja, na kuomba; ndipo nitasikia kutoka Mbinguni." Ewe Mungu, yasikie maombi ya watoto Wako usiku huu, kutoka Mbinguni. Tuma Roho Mtakatifu juu ya wasikilizaji hawa, kama upepo wa nguvu ukienda kasi. Nasi tunawaleta watu hawa mbele za Mungu.

107 Shetani, umeshindwa. Wewe ni kiumbe kilichoshindwa. Yesu Kristo alikushinda pale Kalvari. Huna nguvu. Wewe ni mdanganyifu. Tunakupa changamoto, usiku huu. Katika Jina la Yesu Kristo, toka kwa watu hawa hapa, enyi maradhi na magonjwa. Na jalia waende, wakiwa huru, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

Haleluya! Mnahisi utukufu wa Mungu! Unahisi maombi yako yakijibiwa. Unaamini Mungu alimjibu huyo mtu anayeketi karibu nawe? Ni wangapi wanaamini jambo hilo? Inueni mikono yenu juu. [Kusanyiko linafurahi — Mh.] Haya basi. Loo, ajabu!

Nampenda, na …

Huku mikono yenu imeinuliwa juu sasa, mwimbieni Yeye, kwa moyo wenu wote.

Sababu alinipenda kwanza …

Je, unamaanisha hilo, kwa moyo wako wote sasa?

108 Ni wangapi wenu wanaojisikia ya kwamba Mungu amesamehe maovu yenu, mambo mliyofanya? "Na tangu usiku huu na kuendelea, Ewe Mwana-Kondoo wa Mungu, naahidi kutembea kwa uadilifu. Nitatembea kwa heshima ya Jina nililoitwa, Mkristo, maisha kama ya Kristo. Nitainua mikono yangu, Mungu. Ninajiweka wakfu upya Kwako, usiku huu. Nitatembea katika Nuru." Amina.

Tutatembea katika Nuru, Nuru nzuri,
Inakuja toka ambako matone ya umande wa rehema yanang'aa;
Angaza kote kutuzunguka, mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.
Tutatembea Nuruni, ni Nuru nzuri sana,
Inakuja toka ambako matone ya umande …

Ambako ameenda kutuandalia mahali.

Angaza kote kutuzunguka, mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.
Njoni, enyi watakatifu wote wa Nuru mkatangaze,
Yesu, Nuru ya ulimwengu;
Kweli na rehema katika Jina Lake,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Tutafanya nini basi?

Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri sana,
Inakuja toka ambako matone ya umande wa rehema yanang'aa;
Angaza kote kutuzunguka, mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Loo, hivi hujisikii umesuguliwa kabisa, unajisikia vizuri? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Loo, jamani! Hebu na tupeane mikono, tunapoimba tena.

Tutatembea Nuruni, Nuru nzuri sana,
Inakuja ambako … (Mungu akubariki, ndugu.) … ya rehema yanang'aa;
Angaza kote kutuzunguka, mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Hebu na tufunge tu macho yetu na kuuvumisha huo. [Ndugu Branham na kusanyiko wanaanza kuuvumisha *Yesu, Nuru Ya Ulimwengu* — Mh.] Tutatenda kama watoto. Sisi ni watoto.

Loo, ni Nuru nzuri sana,

Na inakuja ambako umande wa rehema yanang'aa;
Loo, angaza kote kutuzunguka, mchana na usiku,
Yesu, Nuru ya ulimwengu.

Hivi hamumpendi Yeye? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]
Imani yangu inakuangalia Wewe,
Wewe Mwana-Kondoo wa Kalva- …

Funga tu macho yako na uuimbe huo. Abuduni katika Roho.
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondoa dhambi zangu zote,
Ee, hebu niache tangu leo
Niwe Wako kabisa!
Wakati ninapopitia maisha yenye utata gizani,
Na majonzi yakiwa yemenizunguka,
Loo, uwe Wewe Mlinzi wangu;
Amuru giza ligeuke kuwa mchana,
Futa woga wa huzuni,
Wala usiniache nipotee
Kutoka kando Yako.

Loo, jamani! Najua mimi ni jamaa tu wa mtindo wa kale. Napenda … Nafikiri hiyo imeshinda uigaji huu wote mpya, uliokatwakatwa, ya dansi za roki, maili milioni moja. Hao washairi wa kale walioandika hizo nyimbo, Roho Mtakatifu aligusa kalamu hiyo, wakaanza kuandika. Loo, jamani! Nawaza juu ya Eddie Perronet na hao wengine wote; watu wakuu! Fanny Crosby:
Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
Sikia kilio changu cha unyenyekevu.

109 Wakati mmoja walikuwa wakijaribu kumpata. Yeye hakufanya—hakufanya kama Mpentekoste Elvis Presley, kuuza haki zake za mzaliwa wa kwanza kwa mchafuko wa Kadilaki. Yeye … Walimjia na kumtaka awatungie—awatungie nyimbo za kilimwengu. Akasema, "Singefanya jambo hilo, hata kidogo."

Wakasema, "Mbona, wewe ni kipofu. Utakapofika Mbinguni, utamjuaje Yeye?"

Aligeuka, uvuvio, kwa hiyo akasema:
Nitamjua, nitamjua,
Na nitasimama kando Yake niliyekombolewa;
Nitamjua, nitajua (Kwa vipi?)
Kwa alama za misumari katika ninii Yake…

Vinginevyo, "Nisipomwona, nitaupapasa mkono Wake."
Nitamjua, nitamjua,
Na nitasimama kando Yake niliyekombolewa;
Nitamjua, nitamjua
Kwa alama za misumari mkononi Mwake.

Je, hilo halikufanyi umpende? Ameenda kutuandalia mahali! "Na kama nikienda na kuandaa mahali, nitarudi tena, kuwapokea Kwangu."

110 Enyi watoto wadogo mlio katika utungu sasa, tiini tena amri za Mungu. Na mchungaji, hapa, kama hakuna hata mmoja wenu aliyebatizwa, maji yatakuwa tayari. Na—na ufuasi wa kanisa, ama cho chote unachotaka kufanya, ama cho chote kile, fanyeni. Kama huna ubatizo, Roho Mtakatifu, huu ndio usiku wa kumpokea. Hivi hamwamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.]

"Loo," unasema, "Ndugu Branham, tumechelewa. Umehubiri kwa muda mrefu sana."

Paulo alihubiri usiku kucha, usiku mmoja, Ujumbe wa namna hii. Na nanii mdogo … Mvulana mmoja akaanguka kutoka ukutani na kujiua. Naye Paulo, aliyepakwa mafuta sana na Ujumbe wa namna ile ile, akaulaza mwili wake juu yake, na uhai ukamrudia tena. Yeye angali ni "Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele."

Hivi hamumpendi Yeye? [Kusanyiko linasema, "Amina." - Mh.] Hebu na tu, mara nyingine tena, huku tumeinua mikono yetu juu, "Nampenda. Nampenda."

Yuko wapi mpiga piano? Hapo, tafadhali, dada, ye yote yule. Tupe sauti ndogo, tafadhali.

Ni wangapi wanampenda Yeye? Inua tu mkono wako juu. Useme, "Kweli nampenda Yeye. Nampenda tu, kwa—kwa moyo wangu wote. Nampenda Yeye."

111 Sasa hebu na tuuimbe tu, kwa utukufu wa Mungu. Sasa, huku macho yetu yamefumbwa, mikono yetu imeinuliwa Mbinguni, "Nampenda Yeye. Nampenda Yeye." Tunaabudu. Unapohubiri, na kukata, na kurarua, na kuvuta namna hiyo, hii ndiyo zeri ambayo Mungu huimimina, huponya tu. "Kuna Zeri huko Gileadi, kwa ajili ya nafsi." Hebu na tuuimbe sasa. Tupe sauti.

Nampenda, nampenda
Kwa sababu Yeye alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Kwenye mti wa Kalvari.

Na kama … "Hivi watu wote watajua ya kwamba ninyi ni wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo, mmoja kwa mwingine." Hiyo ni kweli. Kama hatuwezi kupendana wale tunaowaona, tutampendaje Mungu Ambaye hatuwezi kumwona?

Ninampenda.

[Ndugu Branham anazungumza na ndugu fulani jukwaani — Mh.] Mungu akubariki. [Ndugu huyo anasema, "Kuwa hapa usiku huu ni heshima halisi kutoka Mbinguni."] Asante, ndugu. ["Ni zuri sana."] Sasa, nafikiri kanisa, kila mmoja, liliimarishwa. Sivyo? ["Naam. Kweli."] Mungu akubariki, Ndugu Boone. Nitalirudishia kusanyiko kwako. Mungu akubariki.

MESSAGE hub online
www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7